JACKPOT BABA LAO!
TZS. 440,981,840
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**ASKOFU GWAJIMA:** Samia na Mpango ni funzo watu kuishi vizuri


Nipashe Spotika
NYOTA 16 WA KOMBE LA DUNIA WATAKAOWINDWA USAJILI 2023
ISIKUPITE

UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Januari 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581185
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ndugu, hospitali waingia mgogoro

**MJAMZITO** avimba mwili wote baada ya upasuaji wa tumbo...

*Endelea ukurasa wa 4*




## SHULE ZAFUNGULIWA

# PM aonya michango, polisi wamulika magari ya shule

UKURASA 2 & 3

## Bima Afya kwa Wote, maboresho Sheria Habari vyasubiriwa

UKURASA 2

**MICHEZO** ROBERTINHO AANZA KAZI, SIMBA WATULIZWA USAJILI UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi jijini Tanga wakijifunza kwa vitendo kilimo cha kisasa maarufu Kilimo Janja wakati wa kambi maalumu ya kujifunza sayansi ya kilimo janja iliyodhaminiwa na mashirika ya Club Rotary Tanga, Robotech Labs na Tanzania Open Innovation (TOIO) kwa ushirikiano wa Jenga Hub kwa usimamizi wa Project Inspire ambao ndio wasimamizi wa Kituo cha Sayansi cha STEM PARK kilichoko mkoani humo mwishoni mwa wiki.
**PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Polisi yatoa angalizo wazazi, madereva wanaobeba wanafunzi

**Maulid Mmbaga na Elizabeth John**

LEO shule za msingi na sekondari zinafunguliwa kwa wanafunzi waliokuwa likizo ya mwezi mmoja kurejea masomoni.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, ameagiza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, waripoti shuleni hata kama hawana sare za shule.

Mwishoni mwa wiki alipozungumza na wananchi mjini Njombe, Mtaka alisema: "Form one (kidato cha kwanza) wale ambao hawana uniform (sare), tumesema waende shuleni, tukasema watoto ambao hawana uniform tunaposema aende shuleni siyo kwamba tumesema sasa kila mzazi mtoto wake aje hana uniform."

Zaidi ya wanafunzi milioni moja wanatarajiwa kujiunga na masomo ya sekondari baada ya kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2022.

Wiki iliyopita, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, alisema kutokana na kuwapo vyumba vya madarasa vya kutosha hakutakuwa na chaguo la pili la wanafunzi wa kidato cha kwanza kama miaka mingine.

Jeshi la Polisi haliko mbali na kufunguliwa kwa shule, likiwataka madereva wanaoendesha vyombo vya moto vinavyobeba wanafunzi wajisimamie badala ya kusimamiwa ili kuhakikisha usalama muda wote.

Limesema ni muhimu kuendeleza utamaduni unaosisitizwa wa kujisimamia na kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani bila kusimamiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, madereva hao wanatakiwa kujiepusha na vitendo vya uzembe vinavyoweza kuhatarisha usalama wa watoto wanaokwenda na kurudi shuleni.

Angalizo hilo limetolewa baada ya shule za msingi na sekondari kwenye maeneo mbalimbali nchini kufunguliwa leo baada ya likizo ya mwezi mmoja.

Misime pia alisema jeshi linawaonya madereva na makondakta wa daladala kuepuka vitendo vinavyowaumiza watoto kimwili au kisaikolojia na kuwanyima haki zao za msingi.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa vile ni takwa la kisheria, kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto wao na kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri kwa watoto hao kwenda shuleni na kurejea nyumbani salama wakiwamo wale wa bweni," alisisitiza.

Misime alisema Jeshi la Polisi kwa mikoa yote limejipanga vizuri kusimamia sheria, ili watoto waendelee kuwa salama waendapo shuleni na kurudi majumbani.

Pia alitoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwalinda watoto, akikumbusha jamii kuwa kumjali na kumlinda mtoto wa mwingine na wa kwako pia wengine watamjali na kumlinda.

*Soma taarifa zaidi Uk. 3

## Bima ya Afya kwa Wote na marekebisho Sheria ya Habari vyasubiriwa

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI za Bunge zinaanza leo huku macho na masikio ya Watanzania yakielekezwa kwenye hatima ya Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022 utakaorudishwa bungeni mwezi ujao.

Wadau wa habari pia wanasubiri utekekelezaji wa ahadi ya serikali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

Novemba 11, mwaka jana, Bunge lilirejesha Muswada wa Sheria ya Bima hiyo kwa Kamati ya Huduma za Maendeleo ya Jamii kwa mashauriano zaidi baada ya kuibuka mjadala mkali bungeni.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, alisema muswada huo unapelekwa kwa kamati na utarudishwa tena baadaye baada ya mashauriano.

Kwa mujibu wa waraka wa Wizara ya Afya unaotoa ufafanuzi juu ya muswada huo, kupitia sheria inayopendekezwa, waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya kupitia kanuni ataweka viwango vya uchangiaji kwa kuzingatia uhitaji wa huduma.

Pia gharama halisi za matibabu na uwezo wa wananchi kuchangia na mapendekezo yaliyoko yatategemea maoni ya wananchi na ridhaa ya mamlaka zingine.

Pia waziri kwa kushauriana na waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, ataainisha viwango vya uchangiaji kwa ajili ya sekta isiyo rasmi, kama itakavyoainishwa katika kanuni, kwa kuzingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya katika utoaji wa kitita cha mafao ya msingi.

Muswada huo pia umewekwa mapendekezo ya watu hawataruhusiwa kupata leseni za udereva na Vitambulisho vya Taifa, huku watakaoshindwa watazuiwa kupata nyaraka hizo.

Kwenye Sheria ya Habari, wadau wanapendekeza kuwapo leseni za muda mrefu za vyombo vya habari, kuondoa jinai, kupunguza mamlaka ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari, Maelezo ikiwamo kufungia vyombo vya habari.

Sheria ya Huduma za Habari, 2016 imetaka kuunda kwa Baraza Huru la Habari, Bodi ya Ithibati na Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Habari.

KATEMANA AUCTION MART & GEN. SUPPLIES
(Auctioneers. Brokers. Debt Collectors. Estate Agents & Commission Agents)

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA KAMPUNI YA MIKOPO YA MKUTI FINANCE LIMITED.

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu, Kampuni ya Mikopo ya **Mkuti Fibance Limited ya Sinza Dar es salaam,** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali zilizo orodheshwa hapa chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo, minada itafanyika mahali zilipo mali hizo, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| Na. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | DHAMANA IPO KWA JINA LA | NYARAKA ILIYOWEKWA NI | SIKU NA TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | VIANO FABIAN KAYOMBO | NYUMBA – MTANDI MASASI MJINI | VIANO FABIAN KAYOMBO | HATI MILIKI YENYE PLOT No. 1841 BLOCK 'B' MTANDI MASASI | SIKU YA IJUMAA TAREHE 27/01/2023 SAA 5:00 ASUBUHI. |
| 2. | GODFREY MICHAEL MWAMVONGO | GARI AINA YA IST – SINZA DSM | GODFREY MICHAEL MWAMVONGO | KADI YA GARI IST T.568 DCL. | SIKU YA JUMAMOSI 04/02/2023. |

**MASHARTI YA MNADA:**

i. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada, salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
ii. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda ho atakuwa amepoteza haki yake, mnada utarudiwa na 25% haitarejeshwa.
iii. Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada.
iv. Mali itauzwa kama ilivyo.
v. Gharama za usajili/ ubadilishwaji umilki ni jukumu la mnunuzi

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-
MKURUGENZI MTENDAJI:
KATEMANA AUCTION MART & GS MOBILE: 0763 452 525 / 0784 988 615 AU
MENEJA – MKUTI FINANCE LIMITED MOBILE: 0677 071 659 / 0765 525 376

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY ADAM ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 201 BZC – SUZUKI CARRY.** Chassis namba **JSAFDA32V001030.** Engine namba **VFN52310.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/10234/2023.**

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA TUNDURU
MAHALI: TUNDURU
MAOMBI NO. 6/ 2022

STIVIN MACHAMBA ELISHA ........MUOMBAJI
DHIDI YA
RAHMA ABDALAH ..............MJIBU MAOMBI

WITO/KUITWA SHAURINI

KWA RAHMA ABDALAH WA TUNDURU
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa Tarehe **16 mwezi 1 mwaka 2023** saa **2:00 ASUBUHI** mbele ya mheshimiwa **J. AYO** Mwenyekiti wa Baraza.

Hivyo unaamriwa kuudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa. Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa baraza hili leo tarehe **12 mwezi 12 mwaka 2022**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TUNDURU

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa aagiza kufuatiliwa mienendo ya wakuu wa shule

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa wilaya na waganga wakuu wa mikoa yote nchini wasimamie maadili kwa watumishi wa sekta ya afya ili fedha zinazotolewa kwenye sekta hiyo ziendane na ubora wa huduma zinazotolewa kwa Watanzania.

Vilevile, ameelekeza wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi na maofisa elimu watembelee shule na kukagua fomu za kujiunga na shule na kujiridhisha hakuna michango ya ovyo.

Amesema serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya afya, ununuzi wa dawa na vifaa tiba, hivyo dhamira yake hiyo ni lazima iendane na ubora wa huduma zinazotolewa wa watumishi katika sekta ya afya.

Majaliwa aliagiza hayo jana alipozungumza na viongozi wa serikali mkoani Ruvuma kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Songea.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya wasimamie upatikanaji wa dawa kutoka Bohari ya Dawa (MSD) na Busket Fund kwa kuwa serikali inatoa fedha za ununuzi wa dawa kila mwezi.

"Hatutaki kusikia malalamiko, serikali kila mwezi inaleta fedha za ununuzi wa dawa, wakuu wa wilaya simamieni hili," Waziri Mkuu aliagiza.

**MICHANGO SHULENI**

Majaliwa pia aliwataka wakuu wa wilaya kwa kushirikiana na wakurugenzi na maofisa elimu wasimamie dhamira ya serikali kutoa elimu bila malipo kaunzia darasa la awali hadi kidato cha sita kwa kutembelea shule na kukagua fomu za kujiunga na shule na kujiridhisha hakuna michango ya ovyo.

Wiki iliyopita, Nipashe ilichapisha ripoti kuhusu michango yenye ukakasi kisheria na hata kukiuka miongozo ya iliyotolewa na serikali katika kuratibu utoaji wa elimu nchini.

Katika ripoti hiyo, Nipashe iliimulika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira iliyoko mkoani Kilimanjaro ambayo fomu zake kwa mwanafunzi aliyejiunga nayo mwaka huu anatakiwa kulipa si chini ya Sh. 295,000/- kwa ajili ya michango mbalimbali.

Baadhi ya michango hiyo ni ambayo kila mwanafunzi wa shule hiyo analazimishwa kuilipa ni ujenzi wa uzio Sh. 100,000/-, motisha kwa walimu Sh. 25,000, masomo wakati wa likizo Sh. 55,000/- na ukarabati wa samani Sh. 15,000/-.

Michango hiyo si tu inakiuka sheria za nchi, bali pia inakinzana na miongozo iliyotolewa na serikali, ikiwamo Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na hata matamko ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kuzuia wanafunzi kulazimishwa kubaki shuleni wakati wa likizo.

Mathalani, Mwongozo wa Serikali kuhusu ugharamiaji wa Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Ada, unaelekeza kutengewe fungu kila mwezi kwa ajili ya ukarabati kwa kila shule, lakini sekondari tajwa ya Ashira inatoza fedha Sh. 15,000 kwa kila mwanafunzi kwa ajili ya ukarabati. Katika mkutano wake wa jana, Waziri Mkuu pia aliagiza kuwapo usimamizi wa shughuli za ustawi wa jamii ikiwamo masuala ya kiuchumi na kwa wafanyabiashara wadogo wa kati na wakubwa.

"Ni lazima tusimamie mwenendo wa uchumi kwenye jamii zetu, shughuli ambazo zinawaingizia kipato wananchi lazima tuzisimamie na kuziimarisha.

"Lazima tufanye tathmini kama tunafanya vizuri au la na lazima tujikite kwenye maeneo yote ikiwamo vijijini," Majaliwa aliagiza.

Waziri Mkuu pia alisema viongozi katika halmashauri zote nchini ni lazima waweke utaratibu na tujikita kuondoa kero za wananchi na kuwa na dhana ya ushirikishwaji kwa kuwaeleza kila kinachofanyika serikalini kwa kutumia vyombo vya habari na kufanya mikutano.

"Lazima tufahamu kero zao na kusimamia kuzitatua," aliagiza Waziri Mkuu na kusisitiza kufanyike utambuzi wa vyanzo vyote vya mapato na kiasi cha fedha kinachoingizwa na kuwataka wenyeviti wa halmashauri zote nchini na mameya kuliwekea nguvu eneo la makusanyo.

Pia alielekeza fedha zote zinazokusanywa kwenye vyanzo vyote ni lazima zipelekwe benki kabla ya kuingizwa kwenye matumizi.

"Ni muhimu pia kukagua matumizi ya vyombo vyetu ya ukusanyaji wa mapato, fanyeni tathmini za mara kwa mara kuhusu mwenendo wa makusanyo," aliagiza.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za jamii na miradi ya maendeleo katika halmashauri, hivyo viongozi kwenye maeneo hayo wanapaswa kusimamia fedha hizo.

"Tunapaswa kusimamia na ni wajibu wetu kufanya hivyo ili tulete matunda yaliyokusudiwa na dhamira ya serikali kwa Watanzania ifikiwe," aliagiza.

# Askofu Gwajima: Samia, Mpango ni funzo watu kuishi vizuri

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, amesema nafasi ya sasa ya Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Philip Mpango inapaswa kuwa funzo la watu kuishi na watu vizuri.

Askofu Gwajima alitoa kauli hiyo jana wakati akihubiri kanisani kwake Ubungo mkoani Dar es Salaam.

"Kuna baadhi ya hatima za watu Mungu ameziunganisha, yule unayemfanyia fujo, unaweza kushangaa kumbe hatima yako imeunganishwa naye. Unaweza ukaishi na mtu ukaona ni wa kawaida tu, ukamchokora, ukamfanyia mambo ya ajabu, kumbe hatima yake imeungana na yako, lakini wewe haujui.

"Nikupe mfano, mimi nina Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa Makamu wa Rais wakati huo Rais wake alikuwa Hayati Dk. John Magufuli.

"Wakati huo Rais Magufuli alimteua Dk. Philip Mpango kuwa Waziri wa Fedha. Kumbe Rais Samia wa sasa na Dk. Mpango walikuwa na hatima ya pamoja, lakini hapo mwanzoni walikuwa wanaona wamechaguliwa na mtu mmoja, ambaye alikuwa Rais Magufuli wakati huo.

"Kumbe mnaweza kuwa mmechaguliwa pamoja, lakini mkawa na hatima ya pamoja, ni vyema kujifunza katika hili. Unaweza kumpiga mtu vita, ukamtukana, ukamdharau, ukambeza, kumbe hatima yenu imeunganishwa na Mungu, uwe mtu wa kiroho au siyo, ni vyema kuangaliana vizuri unapowasemesha watu, hata kama wamekosea, zungumza nao kwa mahesabu, hatima yako na wao zinaweza kuwa zimeunganishwa na Mungu bila wewe kujua," alifafanua.

Askofu Gwajima pia alisema ni vyema kuishi na watu vizuri kwa sababu hao ndiyo wanaweza kuwa wamebeba hatima ya maisha yako ya kesho au baadaye.

"Unaona leo Rais Samia amemchagua Dk. Mpango kuwa makamu wake. Je, angekuwa amemfanyia longolongo, angekuwa wapi sasa hivi? Ishi na watu vizuri, watendee watu mambo mema, watendee watu kwa staha, usiropoke, usikurupuke, yule unayemkoromea au kumkurupukia iko siku anaweza kuwa bosi wako au njia ya kuelekea hatima yako.

"Iko siku anaweza kuwa daraja la kuelekea kesho yako iliyobomoka, ishi na watu kwa tahadhari. Yule unayemkoromea anaweza kujikuta amelazimika kuwa daraja lako kuelekea ustawi wako.

"Hata yule unayetaka kumtukana au kumkoromea, kumwaibisha au kumng`ong`a, ninakushauri ahirisha maana tumbo la kesho limeficha mambo yasiyotarajiwa.

"Tumbo la kesho limeficha matukio usiyotarajia, unaweza kumwona mtu ni wa kawaida, lakini kumbe ndiye huyo amebeba hatima yako hata kama ni miaka mingi ijayo baadaye.

"Inaweza kutokea uliyemwona dhaifu, akageuka kuwa baunsa na wewe uliye baunsa ukageuka kuwa dhaifu. Kila unayemwona ishi naye kana kwamba utamhitaji kesho kwa sababu kesho hiyo imeficha mambo usiyoyatarajia," alisisitiza.

Askofu Gwajima alisema ni vyema kuwatendea watu sawa bila kuangalia rangi, kabila wala hali zao zozote.

"Wembamba wa leo ni wanene wa kesho, wafupi wa leo ni warefu wa kesho, dhaifu wa leo ni baunsa wa kesho, ishi na watu kwa namna nzuri, wathamini watu wote na uwatendee wote sawa bila kujali dini, rangi, makabila yao, elimu zao kwa sababu hujajua kesho watakuwa kina nani. Yule unayemkanyaga ndani ya daladala hujui kesho atakuwa nani," alionya.

Alisema ni vyema watu kujifunza kulizungumzia vizuri taifa, viongozi pamoja na watu unaoishi au kufanya nao kazi.

"Ni afya kumzungumzia mtu vizuri, hata nchi ni vyema watu wakajifunza kuizungumzia vizuri. Nchi tuliyopewa ndiyo hii, hatuna nyingine.

"Sisi ni Watanzania peke yake, ni lazima tujifunze kuizungumzia vizuri na hata viongozi wake kuwazungumzia vizuri, hata unaofanya nao kazi unatakiwa uwazungumzie vizuri kwa sababu hujui kesho italeta nini kwa sababu imeficha mambo mengi. "Yule aliyekulia kwako hujui kesho atakuwa nani, usimpuuze ilimradi yuko hai," alisema.




**Ni kosa kisheria kutumia laini ambayo haijahakikiwa**

Piga *106#, chagua 5 kisha chagua 1 kuhakiki namba kuu au chagua 2 kuhakiki namba za ziada au tembelea duka au Wakala wa mtandao wako kuepuka Laini yako kufungiwa.

Imetolewa na:

airtel · halotel · TTCL · smile · vodacom · tigo

Kwa kushirikiana na:

17218902



Rais mstaafu wa Zanzibar, Amaan Abeid Karume (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Mitaji wa Benki ya Azania, Gilbert Mwandimila (kushoto), alipotembelea banda la Benki ya Azania katika maonesho ya tisa ya Biashara Zanzibar yanayoendelea viwanja vya Maisara Mjini Unguja. Wengine ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar, Ali Juma Khamis (wa pili kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrissa K. Mustafa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugu, Hospitali ya Rufani Mkoa waingia katika mgogoro

**Na Jumanne Juma**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) imeingia katika mgogoro na familia ya Rahma Matola, wakazi wa Mtaa wa Mtakuja, Kata ya Makorora mkoani Tanga kutokana na kile walichodai ndugu yao kutopatiwa matibabu stahiki.

Vilevile, kutokana na hali hiyo wamedai waliamua kumhamishia ndugu yao Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambako hadi sasa kuna deni la Sh. milioni nne ambalo wanaitaka Hospitali ya Bombo kulilipa.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, mume wa Rahma, Akida Akida alidai mke wake alilazwa Hospitali ya Bombo Novemba 11, mwaka jana, kwa ajili ya matibabu lakini baadaye ilibidi afanyiwe upasuaji kwenye tumbo.

Alidai kuwa mkewe alikuwa mjamzito wa miezi saba na baada ya kupimwa, daktari wa Bombo alishauri afanyiwe upasuaji ambao ulifanyika Novemba 15, mwaka jana.

"Mke wangu huwa anajifungua kwa upasuaji, baada ya upasuaji, walibaini kiumbe kilishafariki dunia, wakamfanyia matibabu wakamshona lakini baada ya siku mbili, hali ilibadilika akavimba mwili mzima. Niliwahoji madaktari walidai ni kawaida kwa mgonjwa wa aina hiyo," alidai.

Akida alidai kuwa hali ya mkewe ilizidi kuwa mbaya kutokana na uvimbe kuongezeka huku akilalamika kuwa na maumivu makali.

"Baada ya muda tulijulishwa kuwa itabidi mgonjwa afanyiwe upasuaji mwingine na Novemba 21 mwaka jana alipasuliwa kwa mara ya pili lakini hali ilizidi kuwa mbaya na safari hii hadi ulimi ulivimba," alidai.

Aliendelea kuwasilisha madai yake kwa ilipotimu Novemba 27, mwaka jana, aliwaomba madaktari wampe mgonjwa rufani ili ampeleke Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi.

"Nilikubaliwa kumchukua mgonjwa ila nikatakiwa kuchangia nauli ya gari la wagonjwa Sh. 350,000 na nitapewa muuguzi mmoja, lakini baadaye walisema gari ni bovu na muuguzi ana mtoto mchanga, niliwaambia niko tayari kukodi gari binafsi ila ninaomba muuguzi na gesi ya mgonjwa (Oksijeni) imsaidie akiwa njiani, lakini sikupewa vyote," alidai.

Akida pia alidai kuwa waliomba kibali cha kumwondoa mgonjwa hospitalini huko, nacho walinyimwa na walipewa kitabu cha kutia saini kuwa waliamua kumchukua mgonjwa kwa hiari yao wenyewe bila ridhaa ya daktari.

Kwa mujibu wa Akida, walimchukua mgonjwa wakampeleka Muhimbili ambako walifika Novemba 28 mwaka jana, lakini hawakupokewa kwa kuwa hawakuwa na kibali kutoka Hospitali ya Bombo.

"Mke wangu alikaa eneo la mapokezi kwa saa nane lakini baada ya majadiliano ya kina kati ya familia na madaktari wa Muhimbili, walimpokea na kumpatia matibabu," alidai.

Akida alidai kuwa kwa gharama za matibabu hadi juzi (Jumamosi) zimefikia Sh. milioni nne na kwamba kwa kuwa anaona kuna uzembe uliofanyika Bombo, Hospitali hiyo ya Rufani ya Mkoa wa Tanga inapaswa kulipa gharama hizo za matibabu Muhimbili.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga, Naima Zakaria alikiri hospitali hiyo kumpokea mgonjwa huyo.

# Bolt yaja na nauli na kamisheni mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bolt imesema itafanya mabadiliko kwenye kamisheni na nauli kulingana na mwongozo mpya wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Kauli hiyo inakuja baada ya Desemba 30 mwaka jana LATRA kutoa notisi kwenye Gazeti la Serikali Na. 7284 kuhusu mwongozo mpya wa bei za usafiri.

Meneja wa Bolt Ukanda wa Afrika Mashariki, Kenneth Micah jana aliishukuru LATRA na mamlaka zinazohusika ambazo zimefanya kazi bila kuchoka kuhakikisha kero zilizotolewa na wadau wa tasnia zinashughulikiwa.

Katika taarifa ya Bolt, Micah alisema wamehakikisha kero zinashughulikiwa ili kuwa ma mafanikio kwa wadau wote.

Alisema kwa kuzingatia kanuni mpya za LATRA kwa wahusika wa taxi mtandao, Bolt itafanya mabadiliko kwenye kamisheni na nauli kulingana na mwongozo mpya wa LATRA.

"Bolt itaendelea kutoa huduma ya uhakika kwa mamia na maelfu ya watumiaji Tanzania Bara, ili waendelee kupata njia nafuu, salama na rahisi ya kuzunguka mjini," alisisitiza.

Alisema LATRA na wadau wengine wakuu katika tasnia hiyo wamekuwa na mikutano kadhaa kutokana na kutolewa kwa agizo la LATRA Na.01/2022 Machi mwaka jana, mamlaka hiyo ikiweka ukomo wa kamisheni ya asilimia 15.

"Bolt ilikubali kutii agizo hilo kwa muda ili kuonyesha nia njema licha ya athari mbaya iliyotokana na upunguzaji wa kamisheni kwenye biashara.

"Hili lilifanyika ili kuunda fursa ya azimio la makubaliano ili kuendeleza sekta ya taxi mtandao nchini," alisema.

Pia alisema Bolt itahakikisha maelfu ya madereva wanaoendesha kwenye jukwaa la kampuni hiyo nchini, wanaendelea kupata fursa za mapato.

"Tutaendelea kushirikiana zaidi na LATRA pamoja na wadau wengine wa tasnia hii, ili kuhakikisha ukuaji wa soko huria na zuri la huduma za usafiri wa taxi mtandao nchini Tanzania," alisema.

# Wanaohama eneo la mgodi wa North Mara waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya watu waliolipwa fidia za mali zao kwenye eneo la Komarera wilayani Tarime mkoani Mara kupisha upanuzi wa shughuli za Mgodi wa Dhahabu wa North Mara, imeongezeka kutoka 4,836 hadi 4,881.

Hatua hiyo ni baada ya kamati ya usuluhishi kuelimisha wananchi waliokuwa wamegoma kuhama, wakakubali kupokea malipo yao kupisha shughuli hizo.

Mpaka sasa Kampuni ya Barrick inayoendesha mgodi huo kwa ubia na serikali kupitia Kampuni ya Twiga Minerals, imetumia Sh. bilioni 21.594 kuwalipa wananchi hao 4,881.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mntenjele ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Usuluhishi iliyoundwa na serikali, alisema mwishoni mwa wiki kuwa wanaendelea kuhamasisha wananchi waliochukua malipo ya fidia za mali zao, kuondoka kwa hiari ili kutokwamisha mgodi kupanua shughuli zake za uchimbaji wa madini.

"Tunawasihi wale ambao tayari wameshachukua fedha za fidia, waondoke ili mgodi uendelee kufanya usafi kwenye eneo hili na hatimaye uendelea kuwekeza.

"Hatubomoi kwa mtu ambaye bado yuko ndani lakini kwa yule ambaye ameshaondoka tunabomoa boma lake," alisema Kanali Mntenjele.

Aliwataka wananchi kuwa makini na watu wanaojaribu kuingiza siasa na kupotosha ukweli wa kinachoendelea kwenye eneo la Komerera.

"Kuna wanasiasa wanaingiza siasa humu, jambo ambalo siyo jema kwa sababu hapa ni uhalisia, mtu analipwa kulingana na kitu kilichokuwapo awali.

"Sasa kama umeendelea kuendeleza wakati katazo lilishafanyika siyo halali. Ukianza kuingiza siasa na mkiwasikiliza wanasiasa mtapoteza muda wenu badala ya kuondoka mwende mkafanye maendeleo kwingine ili mgodi nao uendelee kufanya shughuli zake.

"Na tuelewe pia kwamba mgodi huu (North Mara) una ubia na serikali kupitia Twiga Minerals. Sasa kuendelea kuwapo kwenye eneo la Komarera, maana yake mnaikwamisha serikali na mnakwamisha mwekezaji asiendelee kufanya kazi zake," alisisitiza Kanali Mntenjele.

Kwa mujibu wa Mthamini wa Serikali, Rashid Magetta, wananchi hao 4,881 ni miongoni mwa wananchi 5,162 walio kwenye orodha ya kulipwa fidia za mali zao mbalimbali zilizokutwa kwenye eneo la Komarera.

Magetta alisema watu wachache ambao baada ya kulipwa fidia za nyumba zao, walikosa uaminifu wakazipangisha kwa wengine kabla ya usafishaji kuanza kwenye eneo hilo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ntarechagini, Kijiji cha Komarera, Marwa Omuko, alisema wananchi hao walielimishwa kuhusu umuhimu wa kuondoka.

"Kwa mfano, bibi yangu baada ya hii kamati kumwelimisha anachostahili kulipwa na asichostahili kulipwa, ameenda amechukua, lakini wengine hawajaenda kuchukua kwa madai kuwa kiwango cha fidia zao ni kidogo kuliko walivyotarajia," alisema Omuko.

Waandishi wa habari wameshuhudia mitambo ya Barrich North Mara ikiendelea kusafisha eneo la Komarera, ikiwa ni pamoja na kuondoa majengo ya watu waliohama baada ya kupokea malipo ya fidia.

TANGAZO

KUELEKEA UFUNGUZI WA SOKO MALINDI

60 MIAKA YA USHIRIKIANO NA MAENDELEO
60 YEARS COOPERATION & DEVELOPMENT

# Maandalizi yakamilika uzinduzi wa diko na soko jipya la samaki la Malindi, Zanzibar


Miundombinu ya Soko jipya la Samaki la Malindi, Zanzibar ikionekana kuwa safi na salama.

**Na Mwandishi Wetu**

Sherehe za ufunguzi za Mradi wa Maendeleo ya Soko jipya la Samaki la Malindi lililopo Zanzibar zinatarajiwa kufanyika Januari 10, 2023.

Sherehe hizo zitaongozwa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi na Balozi wa Japan nchini, Yasushi Mikawa.

Mradi huo umetekelezwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ambalo jukumu lake kubwa ni kusimamia misaada ya Serikali ya Japan kwa nchi nyingine duniani kote.

Eneo la Malindi si tu bandari kubwa ya uvuvi visiwani humo lakini pia kitovu cha uuzaji wa bidhaa za baharini likinufaisha Manispaa za Zanzibar na na maeneo mengine.

Kabla ya ujenzi wa soko hilo, eneo la uvuvi, maegesho ya vyombo vya uvuvi vifaa vya upakuaji na soko vilivyo karibu na eneo hilo vilikuwa vimeharibika hali iliyozuia ushushaji salama wa samaki pamoja na maandalizi ya safari za uvuvi, na jambo hilo kuathiri vibaya uchumi wa Zanzibar, ambao kwa kiasi kikubwa unategemea sekta ya uvuvi.

Kwa hiyo, kutokana na ombi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Japani kupitia JICA imetoa msaada ambao unalenga kuboresha soko hilo jipya, unaogharimu kiasi cha JPY milioni 1,353 (Takriban Sh22.75 bilioni).

Mradi unajumuisha vifaa vya ushushaji na ukuta wa bahari, vifaa vya mauzo ya jumla (mnada) na vya rejareja.

Mradi huo umetekelezwa na Mkandarasi wa Kijapani RINKAI NISSAN CONSTRUCTION CO., LTD, na mkandarasi mshauri wa Fisheries Engineering Co., Ltd na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar (MBEF).

Katika miaka 60 ya ushirikiano tangu 1962, JICA imesaidia sekta ya uvuvi tangu miaka ya 1970. Soko hilo ni la tatu la samaki kupitia msaada wa JICA, na mradi wa kwanza wa JICA kwa sekta ya uvuvi Zanzibar.


Miradi hii ya ushirikiano baina ya Japan na Tanzania inaonyesha mfano wa "miundombinu yenye ubora wa hali ya juu", ambayo ni msingi wa maendeleo jumuishi kwa watu wote wa Zanzibar.

Soko jipya la Samaki la Malindi litakuwa safi na salama kwa wadau wote wa sekta ya uvuvi. Soko hilo litatoa eneo salama kwa karibu boti 400 za uvuvi, usafi na mazingira bora ya kazi kwa watumiaji 6,500 kama vile wavuvi, wapagazi, madalali, wachuuzi na hivyo kuchangia upatikanaji wa samaki wenye ubora wa hali ya juu kwa wananchi wa Zanzibar.

Mmoja wa wadau wa soko hili, alisema kuwa, anatarajia kupata ajira kutoka katika soko hilo jipya. "Mradi huo ni mkombozi kwa wananchi wa Zanzibar kwani unatoa fursa ya kujiajiri na ujasiriamali" alibainisha.

Miundombinu iliyokamilika ya soko hilo ina uwezo wa kuhudumia meli nyingi zaidi za uvuvi, kutoa ajira zaidi kwa watu katika sekta hiyo, na kuongeza mapato ya wadau katika minyororo ya thamani ya uvuvi, na hivyo kufungua fursa ya uchumi wa Bluu na faida zake. Mradi huu unatajwa kukidhi mahitaji yote ya msingi katika shughuli za uvuvi Zanzibar.


Muonekano wa ndani wa soko. Mnada unatarajiwa kufanyika hapa.


Ghorofa ya kwanza ya jengo la soko hilo.


Muonekano wa Soko la Samaki la Malindi kabla ya mradi wa JICA. Asilimia 95 ya watumiaji wa soko hilo walipata majeraha kutokana na changamoto zilizokuwepo kabla ya mradi.

17206602

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Waamuzi Bara wameshindikana, wachezaji sasa chukueni hatua

**WAAMUZI** ni sehemu muhimu kwenye mchezo hasa kutokana na kusimamia sheria 17 za mpira wa miguu ambao unafuatiliwa na watu wengi zaidi duniani, hivyo ipo wazi kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara imekuwa kwenye ushindani mkubwa na kila siku hatua moja inapigwa kuyafuata matarajio.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mechi ambazo haki imetoweka kutokana na waamuzi kushindwa kusimamia vema sheria hizo kwa usawa. Makosa yapo kwa wachezaji na waamuzi lakini isiwe kwa kurudia mara kwa mara hasa kwa wakati huu ambao timu ikikosa pointi hata moja inaachwa kabisa kwenye mbio za ubingwa, kumaliza nafasi za juu na kuepuka kushuka daraja.

Katika hili, kwa kuwa mara nyingi jicho la watazamaji ama mashabiki huwaangukia zaidi waamuzi, sisi tunaona ni wakati sasa kwa wachezaji wenyewe kwa wenyewe kuona umuhimu wa kulindana afya zao ili kila mmoja aweze kufikia matarajio yake na ya timu kwa ujumla.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba kwenye mechi ambazo zimepita kuna rafu mbaya ambazo zimewasababishia baadhi ya wachezaji kukaa chumba cha majeruhi wakiuguza majeraha yao kutokana na tu maamuzi mabovu ya waamuzi kwa kushindwa kuchuakua hatua mapema uwanjani.

Matokeo yake, Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), inakuwa ikiishia kupelekana kwenye kamati ya maamuzi na matokeo yake baadhi kufungiwa, wakati huo kuna klabu ambazo tayari zimeshaathirika kwa kupoteza alama ama wachezaji wake kuwa majeruhi.

Pamoja na adhabu hizo, bado makosa yanayofanywa na waamuzi ni yale yale kila uchao, hivyo umefika wakati sasa wa kuwataka wachezaji kutafakari kwa kina zaidi kabla ya kucheza rafu zakuumizana zisizo na maana uwanjani.

Hilo litawafanya wazidi kupata kile kilicho bora na kwa namna soka linavyozidi kukua umakini wao utawapa thamani na kuwa bora kwenye kazi yao, na kuepusha kelele kwa waamuzi ambao wamekuwa wakisemwa kila uchao.

Kila kitu kinawezekana ni suala la muda na kila mmoja kuchukua hatua kwa kujiuliza kwanza kama rafu anayomchezea mwanzeke angefanyiwa yeye ingekuwa sawa?

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba tunatamani kuona mpira ukichezwa na 'ball' ikitembea na si kushuhudia viatu na rafu mbaya zisizo na afya kwa wachezaji uwanjani.

Tunatambua mambo mengi uwanjani hufanyika kwa kasi zaidi jambo ambalo mara nyingine huwa vigumu kwa mwamuzi kuyatambua ndiyo maana wenzetu waliopiga hatua kisoka duniani wamkuja na Teknolojia ya Kumsaidia Mwamuzi, VAR.

Lakini licha ya uwapo wa VAR bado makosa hayaishi na baadhi yamekuwa yakionekana. Kwenye Ligi Kuu Tanzania kwa sasa waamuzi wanaonekana wao kazi yao ni kuchezesha mechi tu na si nyingine. Waamuzi hawalindi afya za wachezaji kwa kuachia rafu za ovyo. Waamuzi wa sasa wanakumbwa na matatizo, kwanza wanaanza kuwa na wasiwasi na mechi, au presha wanapochezesha kuliko wachezaji wenyewe wanaocheza jambo ambalo husababisha kuegemea upande mmoja.

Tunadhani pia wanashindwa kujiamini wao wenyewe kwa sababu wanazozijua, kwani mwamuzi anatakiwa kuchezesha kwa haki na sio kuchezesha kwa wasiwasi na kufumbia macho rafu zisizo na maana.

Ikumbukwe pia wachezaji wanapoona mwamuzi hawalindi, hawawezi kuwa huru kutoa burudani kwa mashabiki, matokeo yake soka linakuwa halina ladha na hatimaye kupoteza watazamani uwanjani, hivyo ni wakati sasa kwa TPLB kulitazama hili kwa jicho la ziada.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mashabiki Simba mwacheni kocha mpya afanye kazi yake

**WAKATI** Kocha Zolan Maki alipoingia Simba alibainisha wachezaji anaowakubali na wale ambao alisema hawapo kwenye mipango yake. Tatizo lilikuja pale baadhi ya wachezaji waliotajwa kuwa hawaoni kama wanaweza kuiletea klabu hiyo tija ni vipenzi vya mashabiki wa klabu hiyo.

Sisemi kwamba ndiyo sababu iliyomfanya kuondoka, ila ilichangia mashabiki wengi wa klabu hiyo kutompenda. Baada ya nafasi yake kukaimiwa na Juma Mgunda, hatimaye ameshuka kocha mwingine, Robertinho Oliveira.

Kwa mara ya kwanza ameitazama mara mbili 'laivu' timu yake kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi. Ni mechi ambazo Simba ilichezesha wachezaji ambao hawapati sana namba kwenye kikosi cha kwanza. Kocha alikuwa jukwaani na akatazama uwezo wa vipaji vya wachezaji wake.

Wanachama na mashabiki wengi wa klabu hiyo hawakubaliani na uwezo wa wachezaji wengi wa kikosi hicho, kocha huyo yeye ameona tofauti.

Kuna baadhi ya wachezaji ambao anasema ni wazuri na kuwashangaza wengi, ila akasema wanakosa vitu vichache ambavyo wanahitaji kurekebishwa.

Kocha huyo akapendezwa na uwezo wa wachezaji wanne. Wa kwanza ni Kibu Denis ambaye wanachama na mashabiki wengi wa Simba kwa sasa hawamkubali. Wengine wanataka aondoke au atolewe kwa mkopo.

Taarifa zinasema viongozi wa Simba waliikataa Geita Gold ambayo ilikuwa ikimtaka mchezaji huyo kwa mkopo. Nadhani viongozi wa klabu hiyo bado kuna kitu wanakiona kama ambavyo kocha huyo amekiona, ambapo hakionwi kwa jicho la tatu na mashabiki wa timu hiyo.

"Nimefurahi kwa umri wake unafaa, nitafanya kazi naye na kuhakikisha anakuwa bora," alisema kocha huyo.

Na waliokuwa naye alidai kuwa akauliza ni raia wa nchi gani, akaambiwa ni Mtanzania na akamsifu kutokana na uwezo wake wa kukaba, nguvu na kutumia miguu yote miwili.

Mchezaji mwingine aliyemtaja kuwa ni mzuri ingawa ana mapungufu kadhaa yanayohitaji kurejebishwa ni Jonas Mkude, akamsifu pia kijana Michael Joseph na beki Kennedy Juma.

Katika wachezaji wote wa Simba waliocheza kwenye Kombe la Mapinduzi inaonekana amevutiwa na wachezaji hao tu.

"Kennedy anakaba kwenye nafasi ni mchezaji ambaye hatumii nguvu anafanya kazi nzuri uwanjani ana umbo zuri na ni mrefu ana kila sifa ya kuitwa beki, napenda timu yenye wachezaji wa aina yake nitaendelea kuwaangalia zaidi nijue na mapungufu yao," alisema kocha huyo.

Inaavyoonekana kocha huyu ni aina ya makocha ambao wana uwezo wa kutengeneza wachezaji na si kufundisha zaidi.

Kuna makocha ambao hutumia wachezaji ambao tayari wapo vizuri na wenye uwezo na viwango vikubwa, lakini hawana uwezo wa kuwatengeneza na kuwarekebisha kutokana na kasoro zao.

Robertinho anaonekana ni mmoja wa makocha ambao anaweza kurekebisha mapungufu ya mchezaji ambaye yeye anamuona ana kitu, ila kuna vitu anavikosa.

Hii inaweza kuwa ni faida kubwa kwa Klabu ya Simba kwani inaweza kusababisha baadhi ya wachezaji ambao walikuwa wanaonekana wamekwisha kuibuka tena.

Kinachotakiwa sasa ni wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuacha mihemko, kuchanganywa na kauli za wapinzani wao, badala yake wamuache kocha huyo afanye kazi yake.

Bahati nzuri tu ni kwamba Robertinho ni kocha maarufu kwenye ukanda huu na amepata mafanikio makubwa akiwa na Klabu ya Rayon Sports ya Rwanda na Vipers ya Uganda, vinginevyo kelele zingekuwa zimeshaanza.

Kama viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba watamuacha kocha huyo kwa muda mrefu, anaweza kuwatengenezea kikosi cha kutisha chenye wachezaji bora, uwezo wa viwango vikubwa tena bila kutumia gharama kubwa.

Ni kocha ambaye anaonekana ana jicho la kujua wachezaji anaweza kusajiliwa hapa hapa Afrika wasio na majina makubwa, lakini wenye viwango vikubwa akatengeneza muunganiko wa hatari kama alivyofanya alikotoka ambako alikuwa na vikosi ambavyo havikuwa na gharama kubwa.

Kama huko alikuwa na wachezaji wa kawaida na akafanya kitu, Simba ambao ina uwezo wa kusajili wachezaji wa daraja la kati Afrika, anaweza kufanya makubwa. Kikubwa msimu ujao yeye ndiye awe na mamlaka ya kukata wachezaji wasiofaa na kuleta ambao anaamini atafanya nao kazi nzuri.

# MATANGAZO

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievement and remain an airline of choice that meets and exceeds customer's expectation in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanian to fill the positions mentioned below;

**1. POSITION: AIRCRAFT TECHNICIAN II – STRUCTURES (5 POSTS)**

**1.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:**
- Must be a holder of Diploma in Mechanical Engineering from recognized institutions.
- Certificates of Vocational Certificate Level III Fitter Mechanics majoring in automobile body repairs will be an added advantage.
- The candidate shall be required to attend a special course on aircraft structural repairs after being employed.

**1.2 DUTIES AND RESPOSIBILITIES:**
- Carry out minor and major repair jobs under supervision.
- Work in workshops, hangar and line maintenance sections under supervision.
- Assist in removal and installation of aircraft components, repair, assembling and testing of aircraft systems.
- Perform any other duties as may be assigned by the supervisor.

**2. POSITION: AIRCRAFT TECHNICIAN II – UPHOLSTERS (3 POSTS)**

**2.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORK EXPERIENCE:**
- Must be a holder of Diploma in Mechanical Engineering from recognized institutions.
- Vocational Certificate Level III Fitter Mechanics majoring in Upholstery manufacturing will be an added advantage.
- The candidate shall be required to attend a special course on sewing upholstery for aircraft cabins.

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**
- Sew upholstery (fabric and leather) onto new aircraft seat covers, carpets, car-tens, etc., according to manufacturer's specifications.
- Carry out upholstery repairs.
- Carry out removal and installation of aircraft seats, seat covers, carpets and other cabin upholstery.
- Perform any other duties as may be assigned by the supervisor.

**3. TERMS AND CONDITIONS:**
Five (5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**
Interested applicants must submit **a dully signed letter** for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)**
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicants from Public Service should route their applications through their employers;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**5. CLOSING DATES:**
Applicants should consider the following closing dates for this post as follows:
**Within 14 days from the first date of this announcement**

Application letters should be directed to the following address: -

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**

**Issued on: January 9, 2023**

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## JOB OPPORTUNITIES

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievement and remain an airline of choice that meets and exceeds customer's expectation in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanian to fill the positions mentioned below;

**1. POSITION: PRINCIPAL PLANNING OFFICER II – (1 POST)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**
- Must have a Master's Degree in one of the following fields; Planning, Project Planning, Statistics, Economics or equivalent qualifications from any recognized Institution
- Must have a Bachelor Degree in one of the following fields; Planning, Project Planning, Statistics, Economics or equivalent qualifications from any recognized Institution
- Must have at least ten (10) years of working experience in related field

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**
- Analyze impact of economic growth in relation with Air Tanzania Company Limited (ATCL) business and operation and advice the Management accordingly;
- Coordinate research on areas which have impact in ATCL business;
- Perform cost benefit analysis to the entire ATCL operation and business;
- Continuously scan the internal and external key success factors and identify opportunities;
- Coordinate preparation of ATCL's business and operation strategies;
- Develop and coordinate implementation of aviation related investment and projects;
- Perform other duties assigned by the supervisor.
- Conducts Performance Review and Appraisal of subordinates and gives feedback respectively.
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

**2. POSITION: PLANNING OFFICER II – (1 POST)**

**2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**
- Must have Bachelor Degree in one of the following fields; Planning, Project Planning, Statistics, Economics or equivalent qualifications from any recognized Institution

**2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**
- Assist in the preparation of plans and budget;
- Gathering information and key in data for projects analysis;
- Solicit information for reports preparation;
- Support data collection for the research and survey;
- Collect and key in data for the business analysis;
- Solicit data for required by aviation regulatory bodies association like TCAA IATA, ICAO, AFRAA; and
- Perform any other duties assigned by the supervisor.
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

**3. TERMS AND CONDITIONS:**
Five (5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**
Interested applicants must submit **a dully signed letter** for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)**
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicants from Public Service should route their applications through their employers;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**5. CLOSING DATES:**
Applicants should consider the following closing dates for this post as follows:
**Within 14 days from the first date of this announcement**

Application letters should be directed to the following address: -

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on: January 9, 2023**

# Serikali yaamua wakazi Zingiziwa kuwa wa Mkoa wa Dar es Salaam

**Na Anthony Ishengoma**

KAMATI ya mawaziri wanane ya kutatua migogoro ya ardhi kati ya vijiji na mitaa 975 imehitimisha kazi yake, baada ya kamati hiyo na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kukutana jana na kukubaliana wananchi wa Kata ya Zingiziwa, mkoani Pwani sasa ni wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema kumekuwapo na migogoro ya mipaka kati ya baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam na Pwani na kuzua taharuki kwa wananchi wa maeneo hayo ikiwamo suala la huduma za msingi zinazotolewa katika mikoa yote miwili.

Waziri Mabula alibainisha kuwa baada ya kuhitimishwa mkoani Dar es Salaam maeneo mengine ambayo Rais wa Tanzania ameridhia yachukuliwe au yagaiwe kwa wananchi kazi ya kuyatambua na kuyawekea mipaka linaendelea katika maeneo hayo.

Dk. Mabula alisema utambuzi wa maeneo hayo utajulikana mwezi Machi mwaka huu na kwa maeneo yatakayokuwa yana mkanganyiko wa mipaka, waziri mwenye dhamana atayapitia na kuyatolea majibu baada ya masuala ya kiutaalamu kufanyiwa kazi.

Aidha, alisema kamati yake imebaini kuna sababu tatu zilizochangia migogoro ya ardhi mojawapo ikiwa ya wananchi kutotii sheria ya kuvamia maeneo ambayo hayaruhusiwi kuingia akiyataja ya hifadhi pamoja na yanayomilikiwa na taasisi mbalimbali ambazo zimeshindwa kuyalinda na hatimaye kuvamiwa na wananchi na kujimilikisha kama mali yao.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya maeneo baadhi ya wananchi wanatumia ardhi kinyume na sheria za kutunza mazingira ikiwamo kutofanya kilimo ndani ya mita sitini ya vyanzo vya maji na watu kuendeleza kilimo katika kingo za mito na maziwa akibainisha kufanya hivyo ni kinyume cha taratibu.

Alisema kamati yake inatoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo maji na kuongeza kuwa kila waziri mwenye dhamana alikuwa akiongea na wananchi kuhusu eneo lake na Rais ameridhia maeneo ya hifadhi ambazo zimekosa sifa kugaiwa kwa wananchi kwa utaratibu maalum uliotolewa na serikali.

Waziri wa TAMISEMI, Angellah Kairuki, katika kikao hicho aliamua wananchi wa Zingiziwa kubakia Mkoa wa Dar es Salaam na kuwataka viongozi wa mkoa huo kujipanga ili kuwatangazia wananchi hao kuwa ni wakazi wa wa Dar es Salaam.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwenda mapema kwa wananchi wa Zingiziwa ili kuwatangazia tamko la serikali wakati taratibu nyingine zikifuata zikiwamo za kutafsiri tamko la kiserikali kuhusu mipaka ili kuondoa mgogoro uliopo kiutawala.

Waziri Kairuki alibainisha kuwa maamuzi yake yamezingatia busara ikiwamo huduma za elimu na masuala mengine kama huduma za sensa, usalama, utaratibu wa uandikishaji anwani za makazi, uzoefu wa maeneo ambayo awali yalikuwa na migogoro ya kiutawala.

Wizara vya Ardhi kwa kushirikiana na wizara za kisekta kwa muda sasa wamekuwa katika zoezi la utatuzi wa migogoro ya ardhi hususani kwa wananchi ambao wamekiuka taratibu za matumizi ya ardhi au kumiliki ardhi bila kuzingatia sheria na sasa kamati hiyo imehitimisha kazi hiyo mkoani Dar es Salaam.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendelo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (katikati), Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (kushoto) na Waziri wa TAMISEMI Angellah Kairuki wakiwa katika mkutano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi wadaiwa chanzo kiwango ufaulu elimu ya msingi kushuka

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KITENDO cha baadhi ya wazazi mkoani Pwani kushawishi wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani yao ya kuhitimu elimu ya msingi ni moja ya sababu zinazotajwa kushuka kwa kiwango cha ufaulu.

Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha maboresho ya elimu kilichofanyika mjini hapo na kuhudhuriwa na maofisa elimu wa wilaya pamoja na walimu wakuu. Mlaki alisema sababu hiyo pamoja na nyingine zimechangia kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2022 kushuka kwa asilimia 1.174 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2021.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni kukabiliwa na msongamano wa wanafunzi hali inayosababisha kitendo cha ufundishaji kuwa kigumu na nyingine ni pamoja na kukosekana kwa chakula cha mchana kwa baadhi ya shule.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu Tawala mkoani Pwani, Zuwena Omari, alielekeza wazazi kupewa elimu kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto huku akiwashauri walimu kuzungumza mara kwa mara na wanafunzi athari ya kufeli.

Omari alisema serikali imejizatiti kutatua vikwazo katika sekta ya elimu kwa kuboresha miundombinu ya madarasa na kuongeza idadi ya walimu maeneo yenye upungufu.

Akizungumzia tatizo la lishe, Katibu Tawala huyo alielekeza uhamasishaji ufanyike kwa jamii kuchangia chakula kwa ajili ya wanafunzi muda wa mchana waweze kumudu kukaa darasani kupambana na kikwazo cha mahudhurio.

Mkoa huo umejipanga kuhakikisha kila halmashauri ina mikakati ya kuondoa alama 'D' na 'E' katika mitihani ya ndani na Mamlaka za Serikali za Vijiji na Kata kushirikishwa kushughulikia utoro wa wanafunzi.

# Waridhia Hifadhi ya Munguli kutunzwa kunufaisha wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Munguli, Kata ya Mwangeza wilayani Mkalama, mkoani Singida wameridhia kutangazwa kuwa Hifadhi ya Msitu wa Munguli wenye ukubwa wa hekta 1,656 ulindwe na kutunzwa ili uweze kuwapatia manufaa.

Wananchi hao wameridhia hayo juzi katika mkutano mkuu wa kijiji uliofanyika kijijini hapo na kuhudhuriwa na viongozi wa Serikali Mkoa wa Singida na mwanasheria.

Ofisa Maliasili Mkoa wa Singida, Charles Kidua, aliwaeleza wananchi umuhimu wa kutangazwa kwa msitu huo katika gazeti la serikali kuwa utawapa manufaa makubwa kwa kuwa ngazi za juu zitautambua na kuwekwa sheria ndogo za usimamizi shirikishi wa msitu huo.

Kidua alitaja faida za utunzaji wa msitu huo kuwa ni kupata fedha kwa kunyonya hewa ya ukaa na kupunguza kero ya kutoa michango ya maendeleo mara kwa mara inapojitokeza.

"Katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyokuwa zamani, lazima kila mtu ajue umuhimu wa hifadhi ya mazingira na utunzaji wa msitu ili wananchi wa Munguli waweze kunufaika na msitu huu kama ilivyo kwa jamii ya Wahadzabe walioko Yaeda Chini, mkoani Manyara," alisema.

Mwanasheria wa Wilaya ya Mkalama, Daud Makendi, aliwataka wananchi kufuata sheria na taratibu ili kuepuka kuingia katika makosa ya kisheria.

"Msitu huu utakapotangazwa kuwa Hifadhi ya Msitu wa Munguli kutakuwa na katazo la kutoingia ndani kufanya shughuli zozote za kibinadamu bila kupata kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika," alisema.

Makendi alisema, mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha sheria ndogo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Sh. 50,000 na isiyozidi Sh. 100,000 ikiwa ni pamoja na kulipa fidia ya uharibifu baada ya tathmini kufanyika au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Katika mkutano huo wananchi waliahidi kuulinda na kutunza msitu huo bila kuvunja sheria ndogo na kuridhia kwa pamoja utangazwe kwenye gazeti la serikali.



# Waongoza utalii walia utitiri wa tozo, kodi

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

CHAMA cha Waongoza Watalii nchini (TATO), kimeitaka serikali kutegua kitendawili cha mkanganyiko wa ukusanyaji tozo na kodi katika sekta ya utalii, ili kudhibiti upotevu wa mapato unaoendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali.

Pendekezo hilo liliwasilishwa mwishoni mwa wiki na chama hicho, wakati wa mkutano wa wadau wa sekta hiyo uliofanyika jijini Arusha, ukiongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana.

Mwenyekiti wa TATO, Willy Chambulo, alisema kama serikali itayapatia ufumbuzi matatizo hayo ni dhahiri kuwa itakuwa imeondoa usumbufu, urasimu na upotevu wa mapato unaoendelea kujitokeza kutokana na wingi wa kodi na tozo zinazotokana na utalii, ambazo hukusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa a Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Tunaishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuiwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii, kusimamia yenyewe makusanyo yote ya tozo na kodi tofauti na ilivyo sasa, ambapo kuna wizara nyingine mbili zinakusanya. "Mfano chanya wa kero zinazochangiwa na mkanganyiko huo wa kodi na tozo ni pamoja na tozo wanazotozwa watalii wanapopita kwenye maeneo ya halmashauri za wilaya, wakati wakiwa njiani kwenda kutazama vivutio mbalimbali katika hifadhi za taifa."

Kwa mujibu wa Chambulo utaratibu wa sasa wa mifumo ya ukusanyaji wa kodi na tozo unaoendelea kufanywa na taasisi nyingi unakwamisha na kuchelewesha utekelezaji wa mikakati ya serikali ya kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania. Zaidi alisisitiza: "Kuna haja ya kuwa na mpango wa pamoja wa kuongeza wageni na kwa kweli suala hili likifanikiwa ulipaji wa kodi utakuwa rahisi. Tunataka Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake ahakikishe masuala yote ya tozo na kodi yanasimamiwa na wizara moja".

Alitaja pendekezo lingine ni maslahi duni wanayopata waongoza watalii, wakiwamo wanaopandisha wageni Mlima Kilimanjaro, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia malipo ya Sh. 5,000 hadi Sh. 10,000.

Alisema malalamiko hayo ya maslahi ya wapagazi katika Mlima Kilimanjaro yamekuwapo kwa zaidi ya miaka 10 sasa na hayajafanyiwa kazi, huku wakipendekeza kuongezwa hadi kufikia Dola za Marekani 15. Alisema kutokana na maslahi hayo duni asilimia kubwa ya waongoza watalii wanakata tamaa ya kuendelea kunufaika na matunda ya utalii na wamekuwa wagumu kutoa mchango wao katika kulinda na kuimarisha rasilimali za utalii.

Baada ya mjadala huo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema amepokea mapendekezo 20 ya wadau wa sekta hiyo, likiwamo la nyongeza ya posho za waongoza watalii na wapagazi kwa siku.

Kuhusu suala la kodi na tozo, Waziri Dk. Chana, alisema amelichukua na ataliwasilisha katika ngazi zinazohusika na suala la mifumo ya tozo na kodi ili lifanyiwe kazi na ikiwezekana mwaka ujao wa fedha lianze kusimamiwa na wizara moja.

# Askofu akemea wasichana wadogo kutumikishwa saluni

**Na Oscar Assenga,** KOROGWE

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Tanga, Maimbo Mndolwa, amesikitishwa na wimbi la wasichana wadogo kukatisha kusoma na kwenda kuajiriwa kwenye saluni za kisasa zinazotoa huduma ya kuchua (massage) katika miji mbalimbali nchini.

Amesema haoni mwanga mbele wa maisha yao kwa kuwa nyingi zimegeuka madanguro na kuvunja ndoa za watu.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ibada maalumu iliyofanyika katika Mji wa Korogwe, alisema hata fedha wanazopata ni kidogo, wazazi wao wamekuwa wakifurahi kutokana na watoto wao kufanya kazi lakini humo wanadhalilishwa na watu wenye ndoa zao.

Askofu Mndolwa alisema wasichana hao wanaharibikiwa kwa sababu wanaoingia katika saluni hizo wanatomaswa tomaswa kuliko wanavyofanyiwa majumbani mwao, huku wakishikwa kuliko wanavyoshikwa na wake zao ikiwamo wakati wakivuliwa nguo.

"Kiukweli watoto wanaofanya kazi huko wanadhalilishwa na watu wenye ndoa zao, wanaharibikiwa humo kwa sababu wanatomaswa tomaswa kuliko wanavyofanyiwa nyumbani mwao, wanashikwa kuliko wanavyofanyiwa nyumbani mwao pia wanavuliwa nguo kuliko wanavyovuliwa wanapokuwa kwao matokeo yake ndoa zinaharibika,"alisema.

Kuhusu maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI, Askofu Mahimbo, alisema hivi sasa ugonjwa huo unawaathiri zaidi vijana wengi wenye umri mdogo na wa kati na unasambaa kwa njia za ushoga, kupitia kwenye shule za bweni.

Alisema mpaka sasa anatafakari na hajui kama wazazi wanajua kuna mambo mabaya yanayoendelea huko shuleni, lakini ukweli ni kwamba shule za kulala zina matatizo makubwa.

Kutokana na hali hiyo aliwaomba wamiliki wa shule za bweni, waweke sehemu za kulinda maadili na kiroho ya watu, huku akitoa angalizo kwa wazazi kwamba watoto wao wanaporudi kutoka shuleni wawafuatilie kwa ukaribu simu wanazotumia ambazo waliwakabidhi.

Askofu Mahimbo pia wazazi wafuatilie hata kile ambacho wamekuwa wakikifanya shuleni kupitia madaftari yao pamoja na wale ambao wamekuwa wakihusiana nao ili kuhakikisha wanawalinda watoto wao.




Kamishna Mkuu wa Wakala wa Misitu nchini (TFS), Prof. Dosantos Silayo, akizungumza na wadau wa sekta ya misitu waliokutana jijini Arusha kujadili changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo. Wa pili kulia (walioakaa) ni Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi Dk. Pindi Chana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Wananchi Mwanga kunufaika na kilimo cha parachichi

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

WANANCHI wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, wanatarajia kunufaika na kilimo cha parachichi baada ya serikali wilayani humo kulitangaza kuwa zao mbadala la kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdalah Mwaipaya, akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki kuhusu mabadiliko hayo, alisema serikali inaamini zao hilo litawaongezea kipato wakulima wa eneo hilo wanaoishi pembezoni mwa safu za milima ya Upare.

"Tayari tumezindua kampeni ya ugawaji miche ya parachichi kwa wananchi wa Kata ya Kilomeni. Niwaombe sana wananchi wa Mwanga, kujikita katika kilimo cha parachichi, ambacho utafiti wake uliofanywa unaonyesha kwamba zao hili linastawi na lina uwezo kukidhi mahitaji ya kibiashara.

"Hata uamuzi wa serikali kuendelea kutafuta wawekezaji, kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo hicho kinawapa nguvu ya kulima zaidi kwa kuwa utaongeza upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi,"alisema.

Diwani wa Kilomeni, Mohamed Mgallah, aliwahimiza wakazi wa kata hiyo, kuchangamkia fursa hiyo kwa kuona umuhimu wa kwenda kwenye kilimo biashara cha parachichi.


"Kata ya Kilomeni ina kaya 700 matarajio yetu kwa awamu hii ya kwanza ni kuzifikia kaya 200 ambapo kila kaya tutaipatia miche ya parachichi 20 kwa lengo la kwenda kuipanda miche hiyo kwenye mashamba yao ili kuanzisha kilimo biashara cha zao hilo," alisema.

Mtaalamu wa Kilimo cha Parachichi, Petro Tumaini, alisema malengo ya wilaya ni kila kaya kuwa angalau na miche ya parachichi 20 itakayowawezesha kujipatia kipato kwani soko la parachichi lipo katika nchi za Asia na Ulaya.

Mmoja wa wa kulima wa Kijiji cha Kilomeni, Erasto Chalila, alisema Kilomeni wana zao la miwa na ndizi kama la kibiashara, hivyo kupata zao la tatu la kibiashara la parachichi litakwenda kuwaongezea kipato wakazi hao na wilaya kwa ujumla.

Tanzania kwa sasa ni nchi ya pili barani Afrika kwa uzalishaji wa parachichi ikiongozwa na nchi ya Kenya na zao hilo limekuwa likichangia pato la taifa zaidi ya shilingi bilioni 27 kwa mwaka.

Kwa sasa Tanzania inauza tunda la parachichi katika nchi ya Ubelgiji, Japan, Switzeland, Hispania, Ujerumani na Falme za Kiarabu na bado uhitaji ni mkubwa kuliko kinachopelekwa.







Watoto wakichunga ng'ombe katika Mlima Tinde wilayani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanafunzi waonywa matumizi dawa za kulevya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wanaoingia kidato cha kwanza katika mwaka wa masomo 2023, wameonywa kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya ikiwa ni sehemu ya kulinda na kuzifikia ndoto zao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Dome Manispaa ya Shinyanga, Solomon Najulwa, alibainisha hayo juzi kwenye kikao chake na wazazi wa mtaa huo kilicholenga kuwahimiza wazazi kuwapeleka shule watoto wao waliofaulu kuingia kidato cha kwanza na kuwatimiza mahitaji yao.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wanafunzi hasa pale wanapohitimu elimu ya darasa la saba, kujiingiza kwenye makundi hatarishi ya uvutaji bangi na dawa za kulevya.

"Wazazi naombeni mfuatilie mienendo ya watoto wenu hasa pale wanapohitimu elimu ya darasa la saba, wanavuta sana bangi na kubwia dawa za kulevya, watahairibikiwa akili na kushindwa kutimiza ndoto zao na kuzalisha vibaka mitaani,"alisema Najulwa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Bugoyi 'A' Manispaa ya Shinyanga, Alex Juma, alisema vijana wengi huvuta bangi shuleni hapo hasa majira ya jioni.

"Ni jambo la kusikitisha sana pale tunapoona mtoto mdogo akivuta bangi na hawaogopi hata mchana kweupe wanakuja maeneo ya shuleni na wengine wamemaliza shule ya msingi mwaka jana tu, nawaomba wazazi tuwasaidie watoto hawa hata wanapotoka nyumbani tuwafuatilie wameelekea wapi," alisema Juma.

Baadhi ya wazazi walisema ugumu wa maisha ndiyo umekuwa ukichangia kushindwa kufuatilia mienendo ya watoto wao, sababu wanahangaika huku na huku ili wapate chochote cha kulisha familia na kuahidi kujitahidi kuwafuatilia, pamoja na kuwapeleka shule watoto wao waliofaulu kidato cha kwanza.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alisema jeshi hilo litaanza msako katika vijiwe vyote ambavyo vinajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya ili kuthibiti vitendo hivyo ambavyo huaribu vijana ambao ni tegemeo la taifa.

# Wazee waiomba serikali kuufuatilia mgodi bubu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wazee mkoani Mwanza wameiomba serikali kuhakikisha inafuatilia shughuli za uchimbaji madini katika mgodi bubu wa dhahabu ulioko katika Kata ya Bupamwa wilayani Kwimba mkoani Mwanza ili kujua kama wanafuata taratibu za serikali.

Wakizungumza katika kikao cha pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo hivi karibuni ikiwa pamoja na mambo mengine waliomba serikali kuendelea kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya serikali ili kufanikisha utendaji ndani ya serikali.

Paul Gambago ni mzee kutoka wilayani Kwimba alisema ndani ya wilaya hiyo kuna watu wanaendesha shughuli za uchimbaji wa madini aina ya dhahabu bila kufuata utaratibu na sheria ikiwa ni pamoja na kukwepa ulipaji kodi kwa serikali hali inayosababisha upotevu wa mapato ndani ya wilaya na mkoa huo.

"Nina uhakika kuwa watu hawa hawalipi mapato katika wilaya yetu vilevile nina imani kuwa hawalipi hata katika ngazi ya mkoa maana machimbo hayo yamekaa kiuficho bila ya kujulikana, hivyo serikali ya mkoa inatakiwa kufanya uchunguzi wa kina juu ya mgodi huo ili uanze kufuata taratibu," alisema. Mjumbe wa Umoja wa Wazee wa Mkoa wa Mwanza, Jacob Mutashi, alisema wazee wa mkoa huo tayari wanaendelea na utaratibu wa kuweka wazee wote pamoja na kutatua matatizo yao wenyewe wakiwa na lengo la kutoipa serikali na wadau wengine mzigo wa kufuatilia matatizo yao. Katibu wa Umoja wa Wazee wa Mkoa wa Mwanza, Lweganwa Mganga, aliiomba serikali ya mkoa huo kuendelea kuwatumia katika maamuzi mbalimbali pamoja na shughuli za kiutendaji.

Alisema licha ya wazee wa mkoani humo kuwa na baadhi ya matatizo yakiwamo ya ulipwaji wa mafao yao tayari wameweka mfumo utakaowasaidia kukusanya wazee wote wenye matatizo na kuyawasilisha katika sehemu husika.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, aliahidi kufuatilia mgodi huo ili kuhakikisha kila mgodi uliopo mkoani humo unafuata taratibu na sheria.

Alisema ndani ya mkoa huo yapo mambo mengi yanayohitaji busara na ushauri wa wazee ili kufikia maamuzi sahihi na yasiyoegemea upande wowote.

# DC aomba chumba gerezani kuwasweka wazazi wakaidi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga imeomba chumba katika Gereza la Kahama kwa ajili ya kuwaweka wazazi ambao watashindwa kuwapeleka watoto wao shuleni waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliyabainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari namna walivyojipanga kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kuanza masomo wanaingia darasani, huku akitoa angalizo juu ya wazazi na walezi watakaoshindwa kuwapekea watoto shule.

Alisema katika kipindi hiki serikali haitokuwa na huruma yoyote kwa wazazi wenye tabia ya kutowapeleka watoto wao shuleni kwa sababu ambazo hazina msingi.

Aidha, alisema madarasa yote yamekamilika na yanasubiria wanafunzi kuanza masomo yao na kuwataka viongozi wa serikali za mitaa na kata kuhakikisha wanafuatilia watoto wote kwenye maeneo yao ya utawala.

"Mwaka huu nimeamua kuomba mapema nafasi pale magereza kwa ajili ya kuwakamata wazazi wote ambao hawatawapeleka watoto hususani wakike waliofaulu darasa la saba kwenda kidato cha kwanza kwa wakati nafanya haya ili kutimiza ndoto za watoto wetu bila kujali aina ya maisha waliyonayo,"alisema Kiswaga.

Hata hivyo aliwataka walimu wakuu kuhakikisha vyumba vyote vya madarasa vilivyojengwa hivi karibuni kutumika na wanafunzi hao na siyo vidato vingine ili kuwapatia motisha wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Nipashe
Spotika



MAWINGA 5 - BORA WA KUSHOTO 2022. 12 - 13



EMILIANO MARTINEZ

# NYOTA 16 WA KOMBE LA DUNIA WATAKAOWINDWA USAJILI 2023

**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la 2022 lilikuwa nafasi kwa wachezaji kote ulimwenguni kujitambulisha kwa hadhira ya kimataifa na sawa kusema wengi wao walichukua fursa hiyo.

Skauti wana majina mengi mapya kwenye rada zao na hilo halipaswi kuwa tofauti kwa makocha kwa mwaka huu. Iwe unatafuta msingi mpya au umempenda mchezaji, sasa ni wakati wa kuwaweka kwenye timu yako.

Makala haya inawachambua wachezaji 10 wa Kombe la Dunia la 2022 ambao watawindwa na makocha mwaka huu.

### #1. AZZEDINE OUNAHI

Nyota wa Morocco, Azzedine Ounahi, ndiye gumzo katika ulimwengu wa soka baada ya michuano yake ya kusisimua.

Takwimu zake bora zinajieleza wazi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

### #2. GONCALO RAMOS

Goncalo Ramos tayari alikuwa kwenye rada za baadhi ya timu za juu kabla ya kufunga hat-trick katika mchezo aliochukua nafasi ya Cristiano Ronaldo.

Nyota huyo wa Benfica mwenye umri wa miaka 21, ana takwimu nzuri na kiwango chake kwenye Kombe la Dunia kimemfanya kuwa sokoni.

### #3. NICOLAS OTAMENDI

Mabeki wachache wa kati walikuwa kwenye kiwango bora zaidi ya Nicolas Otamendi mwenye umri wa miaka 34.

Mchezaji huyo wa Benfica bado ni mmoja wa mabeki bora zaidi kwenye mchezo huo, na kiwango chake kinamfanya kuwa kwenye rada za timu nyingi.

Umri wake na mkataba wake unaomalizika, unamwacha Otamendi akiwa na thamani kubwa sokoni.

### #4. ENZO FERNANDEZ

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 21, ni kiungo wa kati ambaye anaweza kuchezea timu yoyote. Fernandez yupo Benfica na ana nafasi nzuri kusajiliwa timu yoyote.

### #5. ALEXIS MAC ALLISTER

Alexis Mac Allister alifurahia moja ya nyakati bora mwaka 2022.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, ni gwiji kwenye safu ya kiungo. Anaweza kuwa nyota wa timu yoyote ndani ya mwaka mmoja au miwili.

### #6. MEHDI TAREMI

Kombe la Dunia kwa Iran halikuwa bora lakini angalau liliweka macho zaidi kwa Mehdi Taremi. Mshambuliaji huyu wa Porto ana takwimu nzuri zaidi.

### #7. YASSINE BOUNOU

Bounou alikuwa mmoja wa walinzi bora kwenye Kombe la Dunia, lakini hilo halijashangaza sana kwa yeyote anayefahamu uchezaji wake akiwa kule Sevilla katika miaka ya hivi karibuni. Raia huyo wa Morocco ni mmoja wa makipa bora katika La Liga na ana uwezo wa kutosha kuichezea timu yoyote.

### #8. JOSIP JURANOVIC

Beki wa kulia wa Celtic, Josip Juranovic, alikuwa na michuano mizuri na ana uhakika wa kujikuta akijiunga na klabu kubwa katika siku za usoni.

### #9. DENZEL DUMFRIES

Mmoja wa mabeki bora wa kulia akiwa na Uholanzi na Inter Milan.

Yeye ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye nafasi yake kutokana na takwimu zake za hali ya juu, na amehakikisha kuwa anafaa kwa ajili ya nafasi ya beki wa pembeni ambayo ameifanya kuwa yake kwa klabu na nchi.

### #10. EMILIANO MARTINEZ

Jamaa asiyejulikana miaka michache iliyopita, Emiliano Martinez, sasa ni mshindi wa tuzo ya golikipa bora wa Kombe la Dunia.

### #11. PEDRO

Kikosi cha Brazil kilikuwa kimejaa majina ya watu wa maarufu, lakini mshambuliaji wa Flamengo, Pedro, alionyesha kiwango bora. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ndiye nyota bora wa Flamengo.

### #12. GIORGIAN DE ARRASCAETA

Mchezaji wa pili kwa ubora kwenye vitabu vya Flamengo, kiungo wa Uruguay, Giorgian de Arrascaeta. Sasa ana umri wa miaka 28, huenda amepitwa na wakati wa kutimiza uwezo wake kamili, lakini De Arrascaeta ni mzuri zaidi ya alivyokuwa.

### #13. DIOGO COSTA

Huenda Diogo Costa hakujifunika kila mara kwa utukufu kwenye Kombe la Dunia, lakini hiyo haimaanishi kwamba hupaswi kuwaniwa na klabu. Akiwa na umri wa miaka 22, Costa tayari ni mchezaji bora ambaye anaweza kuichezea timu yoyote.

### #14. MOHAMMED KUDUS

Kiungo wa kati wa Ghana Mohammed Kudus ni mmoja wa watu wengi wenye vipaji vya juu kule Ajax ambao wako tayari kuchukua hatua inayofuata. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ni kiungo mwingine mzuri ambaye anaweza kuanza mara moja kwa timu yoyote.

### #15. ADRIEN RABIOT

Kwa mshtuko wa mashabiki wengi wa Juventus, Adrien Rabiot alikuwa mmoja wa viungo bora kwenye Kombe la Dunia.

Mfaransa huyo amevutia watu wengi anapokaribia mwisho wa mkataba wake, kwa hivyo anaweza kuwaniwa na klabu yoyote kwa sasa.

### #16. GUILLERMO OCHOA

Mchezaji nyota wa Kombe la Dunia, Guillermo Ochoa anapenda kujitokeza kwenye hatua kubwa zaidi na kwa kweli bado ana uwezo wa kutosha kufanya hivyo katika ngazi ya klabu pia. Raia huyo wa Mexico mwenye umri wa miaka 36, bado ana kiwango bora zaidi golini.

## ISIKUPITE

NI wachezaji watatu tu ambao wamefunga mabao 30 na zaidi kwenye Ligue 1 tangu kuanza kwa msimu uliopita, ambao ni Kylian Mbappe wa PSG (41), Wissam Ben Yedder wa Monaco(32) na Martin Terrier wa Rennes (30).



Extra Time

# MAWINGA 5 - BORA WA KUSHOTO 2022



CODY GAKPO

**LONDON,** England

SIKU zimepita wakati mawinga wa kushoto walikuwa mashine za kuvuka bila kuchoka. Mawinga wa kushoto wa zama za kisasa ni hodari zaidi, wenye uwezo wa kufanya mengi zaidi.

Wengi wa mawinga wa sasa wa kushoto wanaocheza kwa kasi kubwa, ni wazuri sana wakiwa na mpira miguuni mwao.

Hapa tunawaangalia mawinga watano bora wa kushoto kwa mwaka 2022, twende sasa...

### #5. RAFAEL LEAO (URENO) - AC MILAN

Winga wa kushoto wa AC Milan, alikuwa mmoja wa wachezaji wao bora katika kampeni yao ya ushindi wa msimu wa 2021-22. Alifunga mabao 11 na kutoa asisti 10 katika michezo 34. Mabao saba na asisti nane zilipatikana katika michezo 19 kati ya Januari na Mei 2022. Leao pia alifunga mara mbili katika mechi nne za Kombe la Italia na mara moja katika mechi nne za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Winga huyu wa kushoto aliyeshinda Serie A msimu wa 2021-22, amekuwa katika kiwango cha kustaajabisha katika msimu wa 2022-23 pia. Katika mechi 20 kwenye mashindano yote, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mara saba na kutoa pasi tisa za mabao.

**Leao hakuanza mchezo wowote kati ya mitano ya Ureno kabla ya kuondolewa na Morocco katika robo fainali ya Kombe la Dunia la 2022. Licha ya kucheza dakika 83 pekee za soka katika mechi tano, alifunga mara mbili.**

### #4. CODY GAKPO (UHOLANZI) - PSV EINDHOVEN

Winga wa kushoto aliyesajiliwa hivi karibuni na Liverpool, Cody Gakpo, alikuwa na mwaka mzuri wa 2022. Alijitangaza kwa mara ya kwanza kwa ulimwengu kwa uchezaji wake akiwa na PSV Eindhoven. Wakati wa Kombe la Dunia la 2022, alithibitisha ni kwa nini watu walikuwa sawa kumsifu kama mmoja wa wachezaji wachanga wanaovutia zaidi Ulaya.

Gakpo alifunga mara sita na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 14 za Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, katika kipindi cha pili cha msimu wa 2021-22. Pia alifunga mara mbili kwenye Kombe la Uholanzi, ikiwa ni pamoja na mara moja katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Ajax kwenye fainali. Kabla ya kujiunga na Liverpool, Gakpo alifunga mabao 13 na kutoa pasi 17 za mabao katika mechi 24 akiwa na PSV Eindhoven msimu wa 2022-23.

Akija kwenye soka la kimataifa, alifunga mara tatu katika mechi tano za Uholanzi, kabla ya Argentina kuwaondoa kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

### #3. NEYMAR (BRAZIL) - PARIS SAINT-GERMAIN

Nyota wa Paris Saint-Germain (PSG) na Mbrazil Neymar alikuwa na mwaka mzuri wa 2022. Winga huyo wa kushoto alijitahidi kujiweka sawa katika kipindi cha kwanza cha mwaka, lakini alikuwa na ufanisi kila alipoitwa. Katika mechi 12 za Ligue 1 kwenye kipindi cha pili cha msimu wa 2021-22 wa Ligue 1, Neymar alifunga mabao 10 na kutoa asisti tatu. Msimu huu, winga huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 30, amewasha moto Ligue 1 na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Amefunga mara 11 na kutoa asisti 10 katika mechi 15 za ligi. Huko Ulaya, amefunga mabao mawili na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi tano.

Neymar ameichezea Brazil mara tatu pekee kwenye Kombe la Dunia 2022, akikosa mechi mbili za hatua ya makundi kutokana na jeraha la kifundo cha mguu. Alifunga mara mbili na kutoa asisti kabla ya 'Selecao' hao kuondolewa na Croatia kwenye robo fainali.

### #2. SADIO MANE (SENEGAL) - LIVERPOOL/BAYERN MUNICH

Winga wa kushoto wa Bayern Munich, Sadio Mane aliwatesa wapinzani kwa kasi yake na kutochoka mwaka wa 2022. Katika mechi ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, fowadi huyo wakati akiwa Liverpool alifunga mara tatu na kutoa asisti katika michezo saba.

Katika msimu wa Ligi Kuu wa 2021-22, alifunga mara tisa na kutoa pasi mbili za mabao kwenye michezo 16 mwaka 2022. Katika nusu fainali ya Kombe la FA, Mane alifunga mabao mawili na kuipeleka timu yake kushinda 3-2 dhidi ya Manchester City. Liverpool iliifunga Chelsea fainali kwa mikwaju ya penalti. Mane pia alicheza fainali ya Kombe la EFL huku Liverpool kwa mara nyingine ikiifunga Chelsea katika mikwaju ya penalti.

Winga huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 30, alijiunga na Bayern Munich msimu wa majira ya joto wa 2022 na amefunga mabao 11 na kutoa asisti nne katika mechi 23 za mashindano yote. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal hakuweza kuisaidia timu yake ya taifa katika Kombe la Dunia 2022 kutokana na kuwa majeruhi.

### #1. VINICIUS JUNIOR (BRAZIL) - REAL MADRID

Winga wa kushoto wa Real Madrid, Vinicius Junior alifurahia mwaka mzuri sana wa 2022. Mbrazil huyo mchanga aliboresha matokeo yake chini ya kocha Carlo Ancelotti na alicheza jukumu muhimu wakati 'Los Blancos' waliponyakua mataji matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, LaLiga na Supercup msimu wa 2021-22. .

Katika kipindi cha pili cha msimu wa 2021-22, Vinicius alifunga mabao mawili na kutoa pasi tatu za mabao katika michezo saba ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Katika LaLiga, alifunga mara saba na kutoa asisti nane kwenye mechi 16. Vinicius pia alifunga mara moja katika mechi mbili za Supercup.

Msimu huu, winga huyo wa kushoto ameibuka mfungaji bora wa 'Los Blancos' hao katika michuano yote. Kwenye LaLiga, ameandikisha mabao sita na kutoa pasi tatu za mabao katika michezo 15, huku pia akifunga mara nne na kutoa pasi za mabao katika mechi sita za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, pia alionyesha cheche za uzuri kwenye Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, akifunga mara moja na kutoa pasi mbili za mabao kabla ya Brazil kutupwa nje kwenye hatua ya robo fainali.

## Nukuu

"Halo watu wangu, mwaka mkuu nyuma yangu, mabadiliko mengi, lakini muhimu zaidi, mabadiliko kwa ubora zaidi. Asante kwa upendo wote unaoendelea na tushikamane mwaka wa 2023. Kama ninavyosema kila mara, mengi yanakuja zaidi!," **Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland akiuaga mwaka 2022 na kuukaribisha 2023**



"Kwangu mimi, Henry (Thierry)ndiye kocha ajaye wa Ubelgiji. Hakuna shaka. Nasema wazi: atakuwa kocha ajaye. Ana heshima ya wachezaji wote, ameshinda kila kitu, anajua kufundisha, anajua tunachotakiwa kufanya ili kufika huko. Anaijua timu, ligi, wafanyakazi. Kwangu mimi ndiye kocha bora kwa timu yetu ya taifa, basi sijui watamchukua nani. Lakini sidhani kama Ubelgiji inapaswa kuanza kutoka mwanzo," **Mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku baada ya Kocha Roberto Martinez kuachia ngazi ya kuinoa timu hiyo ya taifa.**



"Unahitaji mtu ambaye anaweza kuwa na mchango na si kuchoma fedha. Tuna timu nzuri. tuna mshambuliaji, Anthony Martial, nina furaha sana na uchezaji wake katika michezo mingi, amekuwa na matokeo mazuri sana. Ukiona dakika zake na mchango wake umekuwa mkubwa," **Kocha Erik ten Hag akisisitiza kwamba, Manchester United haitachoma fedha kusajili mshambuliaji mpya Januari hii.**





YOURI TIELEMANS

# NYOTA BORA WANAOWEZA KUSAINI MIKATABA JANUARI

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili la Januari 2023 lipo wazi na klabu zitatafuta kusajili mchezaji mmoja au wawili ili kuimarisha kikosi chao katikati ya msimu huu.

Hata hivyo, pia kuna baadhi ya wachezaji ambao wamebakiza miezi sita pekee katika mikataba yao ya sasa na wanaweza kusainiwa kwa makubaliano ya awali ya mkataba Januari.

Makubaliano ya awali ya mkataba ni kipengele muhimu kwani huruhusu klabu kuanza haraka biashara yao ya uhamisho wa majira ya joto kwa kumsajili mchezaji Januari.

Zaidi ya hayo, kusajili wachezaji wa kiwango cha juu kwa uhamisho wa bure ni bonasi kubwa, kwani huondoa hitaji la kufanya mazungumzo ya aina yoyote ya ada na klabu nyingine.

Ingawa mikataba kama hiyo mara nyingi hujumuisha bonasi kubwa za usajili kwa wachezaji, mwishowe hulipa kulingana na ubora wa mchezaji.

Kwa maelezo hayo, hebu tuangalie wachezaji watano bora ambao wanaweza kusajiliwa kwa makubaliano ya awali ya mkataba Januari hiii...

### #5. MEMPHIS DEPAY

Kiwango cha Memphis Depay kwa kiasi fulani kimepanda katika miaka michache iliyopita. Depay alicheza katika michezo yote mitano akiwa na Uholanzi kwenye Kombe la Dunia na kufunga bao moja, ingawa mchango wake ulikuwa zaidi ya hilo. Harakati zake za nje ya mpira, uwezo wa kuungana na wachezaji katika nafasi ulikuwa mzuri.

Hata hivyo, vipengele hivi si vitu ambavyo mashabiki wa Barcelona wamekuwa wakivijua, kwani Depay amepunguza hali mbaya Nou Camp tangu kuwasili kwake.

Zaidi ya hayo, Xavi hampendelei mshambuliaji huyo na anaweza kuwa tayari kumwacha aondoke kwa uhamisho wa bure katika msimu ujao wa majira ya joto. Lakini hii haimaanishi kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hawezi kuwa nyenzo muhimu kwa upande mwingine wowote wa juu barani Ulaya.

Mabao yake 76 na asisti 55 katika mechi 178 alizochezea Olympique Lyon ni uthibitisho kwamba anaweza kuwa mchezaji bora.

Kwa hivyo, ikiwa imesalia miezi sita tu kwenye mkataba wake, klabu nyingine zinaweza kumsaini Depay kwa makubaliano ya awali ya mkataba katika dirisha la usajili la msimu huu wa baridi.

### #4. YANN SOMMER

Yann Sommer amekuwa mmoja wa magolikipa bora zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, tangu ajiunge na Borussia Mochengladbach mwaka 2014.

Mlinda mlango huyo amecheza mechi 335 kwenye klabu hiyo ya Ujerumani katika kipindi cha miaka nane iliyopita. Kwa hiyo, amekuwa na wastani wa michezo 40 kwa msimu na amedumisha kiwango cha juu mfululizo.

Uchezaji wake katika Timu ya Taifa ya Uswisi pia umekuwa wa kupongezwa. Kwa hivyo ni kitendawili kwa nini mchezaji huyo bado hajahamia klabu kubwa.

Bila kujali, ikiwa imesalia miezi sita pekee katika mkataba wake wa sasa, Sommer atakuwa anaweza kusani katika klabu yoyote.

Hata hivyo, kutokana na uwezekano wa ushindani kuwa mkubwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, kumsajili kwa makubaliano ya awali ya mkataba Januari hii itakuwa ni hatua nzuri zaidi.

### #3. STEFAN DE VRIJ

Stefan de Vrij amekuwa mmoja wa walinzi bora katika soka la dunia kwa miaka kadhaa iliyopita. Amekuwa na ushawishi mkubwa katika maendeleo ya Inter Milan katika miaka ya hivi karibuni, haswa ukizingatia aina yao ya uchezaji. 'Nerazzuri' ni wazuri na wazuri katika kutoka nyuma, kwa hisani ya mabeki kama De Vrij kuwa na ufundi wa kupiga pasi kutoka nyuma.

Nyota huyo wa Uholanzi pia ni bora katika kutengeneza pasi. Kwa hiyo, licha ya uzoefu wake mwingi na maarifa, inashangaza kwa nini Inter Milan bado hawajampa mkataba mpya.

Kwa hvyo, wakati huu wa dirisha hili la Januari, De Vrij anaweza kuondoka Inter Milan bure.

### #2. YOURI TIELEMANS

Mbelgiji huyu amecheza katika mifumo tofauti katika Klabu ya Leicester City, jambo ambalo limemwezesha kuwa kiungo kamili. Kiwango cha kazi yake ya ulinzi, akili ya ubunifu, na uwezo wa kuamuru kasi ya mchezo umekuwa wa thamani sana.

Ongeza kwa ukweli kwamba bado hajafikia kilele chake cha kitaaluma, bila kusahau kwamba kujiunga na moja ya klabu kubwa duniani.

Ingawa kulikuwa na uvumi kuhusu yeye kuondoka msimu wa joto uliopita, alikaa kwenye Uwanja wa King Power. Hata hivyo, ikiwa imesalia miezi sita pekee katika mkataba wake, klabu nyingi zitakuwa na nia ya kumsajili bure kupitia makubaliano ya awali ya mkataba.

Kwa hiyo, Leicester italazimika kuchukua hatua haraka ikiwa wana matumaini yoyote ya kuweka mchezaji wao bora katika klabu baada ya 2023.

### #1. N'GOLO KANTE

Katika kipindi cha nusu muongo uliopita, N'Golo Kante amekuwa mmoja wa viungo bora zaidi duniani. Nyota huyo wa Chelsea ameshinda kila taji la ndani akiwa na klabu hiyo, ukiondoa Kombe la Carabao. Mchango wake katika ushindi huo pia umekuwa mkubwa, huku mchezaji huyo mara nyingi akitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika michezo muhimu.

Hata hivyo, Kante yuko katika hatari ya kuumia sana kwa sasa na amekosa mechi nyingi kwa miaka miwili iliyopita.

Ingawa bado ndiye mchezaji bora zaidi uwanjani anapocheza, kumekuwa na visa vichache hivi karibuni. Zaidi ya hayo, huku wamiliki wapya wa Chelsea wakiunda kikosi cha vijana, kumwacha Kante kuondoka kunaweza kuwa hatua sahihi.

N'Golo Kante anaripotiwa kutaka kusaini mkataba wa awali na Barcelona mwezi huu kwani mkataba wake Chelsea utakamilika msimu huu wa majira ya joto.

Lakini kupoteza kwa Chelsea kunaweza kuwa faida ya mtu mwingine. Huku Kante akiwa bado na angalau miaka kadhaa mizuri iliyosalia ndani yake, kumsajili kwa uhamisho wa bure kunaweza kuwa na faida.

**JE, WAJUA?**



UHAMISHO wa Philippe Coutinho kutoka Liverpool kwenda Barcelona uliogharimu euro milioni 135, ndio unaoshikilia rekodi ya kuwa wa gharama kubwa zaidi katika historia ya uhamisho majira ya baridi, ukifuatiwa na Virgil van Dijk kutoka Southampton kwenda Liverpool (euro milioni 85) na wa Dusan Vlahovic kutoka Fiorentina kwenda Juventus kwa euro milioni 82.



## Mamia wajitokeza kununua nyumba za kisasa NHC

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

MAMIA ya wananchi wamejitokeza kununua nyumba za kisasa za makazi zinazoendelea kujengwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika viwanja vya Tanganyika Pakers jijini Dar es Salaam.

Idadi kubwa ya wananchi hao wamejitokeza kununua nyumba hizo mapema hata kabla ya kukamilika kwa mradi.

Akizungumza na Nipashe jijini hapo katika mahojiani maalumu, Meneja Uhusiano wa Umma na Habari wa NHC, Muungano Saguya, alisema katika mradi huo wa Kawe jumla ya nyumba 560 zinajengwa katika awamu ya kwanza.

"Hadi jana (Jumapili) takribani nyumba 320 zilikuwa zimeuzwa kwa wananchi mbalimbali ambao wameamua kulipia nyumba hizo mapema kabla hata ya kukamilika kwa ujenzi wake, mauzo ambayo ni sawa na asilimia 57," alisema.

Saguya alifahamisha kuwa kwa sasa jumla ya nyumba 239 zimebakia katika orodha ya mauzo.

Alisema kutokana na mwendo mzuri wa ununuzi wa nyumba hizo, kwa wastani wa asilimia 37, tangu Novemba 1, mwaka jana NHC ilipofungua rasmi dirisha la ununuzi wa majengo hayo.

"Hapo awali, mradi ulikuwa na nia ya kujenga nyumba 400 katika mtindo wa ghorofa 10 tofauti lakini kutokana na ongezeko la mahitaji, tuliamua kuongeza idadi hadi angalau nyumba 560 ili kuhudumia Watanzania wengi zaidi," alisema.

Alisema kutokana na nia ya dhati ya shirika kuwasaidia Watanzania wa kawaida kumudu kumiliki nyumba za kisasa za makazi, NHC inaziuza nyumba hizo kwa bei ya kizalendo.

"Ni matarajio yetu kuwa baada ya kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi, tutaanza ujenzi wa awamu ya pili wa nyumba nyingine katika eneo la Kawe, ili kuwahudumia wananchi wengi zaidi," aliongeza.

Alisema asilimia 50 ya nyumba hizo zitajengwa jijini Dar es Salaam wakati asilimia 20 zitajengwa katika mkoani Dodoma na asilimia 30 iliyobaki itapelekwa mikoa mingine.

NHC linatekeleza mradi mkubwa ujulikanao kama 'Samia Housing Scheme' wenye thamani ya Shilingi bilioni 466 unaolenga kujenga takribani nyumba 5,000 za bei nafuu katika maeneo mbalimbali ndani ya mikoa tofauti, ikiwamo jijini Dar es Salaam katika viwanja vya Tanganyika Packers.

# Bashe awatoa hofu wakulima utoaji mbolea ya ruzuku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema kero zilizoko kwenye mfumo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea ni za muda mfupi kwani mfumo huo umeanzishwa mwaka huu, kwamba utaendelea kuboreshwa.

Aliyasema hayo alipofanya ziara mkoani hapo kwa dhumuni ya kuangalia namna ya utoaji wa mbolea za ruzuku unavyofanyika.

Alisema mfumo ni mzuri kwa kuwa unamtambua mkulima anayelengwa kunufaika na mbolea za ruzuku tofauti na mfumo wa vocha uliotumika miaka ya nyuma na kunufaisha wafanyabiashara wa mbolea pekee.

"Mfumo wa mbolea ya ruzuku una matatizo yake lakini hatuwezi kurudi nyuma sababu unamtambua mkulima," alisema Bashe.

Waziri Bashe alifafanua kuwa lengo la Rais Samia Suluhu Hassan ni kumlipia ruzuku mkulima na kwa kutumia mfumo huo serikali italipia mbolea iliyomfikia mkulima na siyo vinginevyo.

Bashe aliwaelekeza wauzaji wa mbolea kuongeza idadi ya watoa huduma za kuuza ili kuweza kuwahudumia wakulima wengi kwa muda mfupi ili kuondoa msongamano.

Pia aliwataka wakulima kuwa na subira na kubainisha kufikia msimu ujao wa kilimo matatizo hayo hayatakuwapo.

"Mateso mnayoyapata ya foleni yatakwisha kuweni wavumilivu wakati serikali inajenga mfumo," alisema Bashe.

Aidha, aliomba uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kila mkoa kuwa waelimishaji wakubwa wa wananchi juu ya kutunza namba zao za utambulisho wa mkulima ili wasirubuniwe na kuziuza kwa mawakala.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na viongozi wa serikali wa Mkoa wa Ruvuma katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Wanafunzi vyuo vikuu watakiwa kuhifadhi, kulinda mazingira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI wa vyuo nchini wametakiwa kuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuhifadhi na kulinda mazingira ili kupambana na mabadiliko tabianchi.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba, wakati akishiriki katika usafi wa mazingira katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma lililoandaliwa na Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu (TAHLISO).

Dk. Komba alimwakilisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Dk. Switbert Mkama.

Alisema usafi ni sehemu ya kuunga mkono utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021.

Hivyo, aliwapongeza wanafunzi hao wa vyuo kwa kuandaa zoezi hilo la usafi ikiwa ni katika kuunga mkono juhudi za serikali za usafi na uhifadhi wa mazingira.

"Kama mnavyofahamu serikali ilishautenga Mkoa wa Dodoma kuwa wa mfano katika masuala ya mazingira, hivyo tunahakikisha tunapanda miti ya kutosha na nyie hapa leo mmeonesha mfano kwa kufanya usafi hospitalini hapa," alisema Dk. Komba.

Mkurugenzi huyo pia alisema ni wakati muafaka kwa wanafunzi wa vyuo kuwarithisha wadogo zao njia za kutunza mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Naye Mkuu wa Idara ya Afya Mazingira Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Paul Mageni, alisema katika kuunga mkono serikali wameanzisha bustani ya miti katika eneo la hospitali hiyo.

Mageni alisema miti iliyopandwa mbali ya kuhifadhi mazingira lakini inawasaidia wananchi wanaopata huduma hospitalini hapo kupata hewa nzuri na matunda.

Viongozi wa TAHLISO kutoka Tanzania Bara na Visiwani walitoa pongezi kwa uongozi wa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa kuwapa wasaa wa kufanya usafi katika eneo hilo.

Hata hivyo, waliwapongeza wanafunzi wa vyuo mbalimbali walioshiriki katika zoezi hilo ambalo ni njia mojawapo ya kuunga mkono serikali katika kuhakikisha mazingira yanakuwa endelevu kwa mustakabali wa taifa.








Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akikabidhi zawadi kwa Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Phillip Mangula, baada ya uzinduzi wa mnara wa Vodacom uliojengwa kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) katika kijiji cha Imalinyi mkoani Njombe jana. Kulia ni Meneja Mauzo wa Vodacom Njombe, Maula Mafuru na Mkurugenzi Mtendaji wa UCSAF, Justina Mashiba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaoishi na VVU wapewa msaada wa baiskeli

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la HJF Medical Research International (HJFMRI), limetoa baiskeli 20 kwa mawakili tiba (watu wanaoishi na virusi vya ukimwi) walio mstari wa mbele kutumia dawa kikamilifu ili waweze kuwafikia wenzao ambao wameacha kutumia dawa katika vituo vya afya 20 vilivyo katika Mkoa wa Mbeya.

Akitoa msaada huo mwishoni mwa wiki kwa niaba ya Mkurugenzi wa Shirika la HJFMRI Tanzania, Dk. Emmanuel Bahemana ambaye ni Mkurugenzi wa Utafiti wa Shirika hilo alisema wametoa msaada huo na zitasambazwa katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya.

Alisema lengo ni kuwasaidia mawakili tiba kuwafikia wenzao waliocha kutumia dawa kwa ajili ya kuwahamasisha waendelee kutumia dawa tiba kwa lengo la kuimarisha afya zao na pia kupunguza uwezekano wa maambukizi mapya.

"Msaada huu ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika kuimarisha utoaji huduma za Virusi vya Ukimwi (VVU) katika Mkoa wa Mbeya. Sisi tunafanya kazi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutekeleza afua mbalimbali za mapambano dhidi ya VVU.

Awali akipokea msaada huo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, aliwapongeza Shirika la HJFMRI kwa kuwa mdau muhimu hususani katika kusaidia mapambano ya VVU kupitia afua mbalimbali.

Alisema kimekuwa kilio cha Mkoa wa Mbeya kuwawezesha mawakili tiba walio katika kila kituo cha afya ili waweze kuzunguka katika maeneo yao na kuwatafuta watu wanaoishi na VVU ambao wameacha kutumia dawa tiba ili kuwarudisha kwenye matibabu.

Mshauri wa Mradi wa Huduma Endelevu na Matunzo kutoka Shirika hilo, Dk. Kalebi Mwilawi, alisema kwa takwimu za mradi zaidi ya mawakili tiba 500, wanaoishi na VVU katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wamepatiwa afua mbalimbali za kupambana na virusi hivyo ikiwamo kujengewa uwezo kuhusu matumizi sahihi ya dawa za kufubaza virusi. Aliongeza kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ndiyo inaoongoza kwa idadi kubwa ya watu walioacha kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU ikifuatiwa na Chunya sababu kubwa ilitajwa kuwa ni kujikita zaidi kwenye shughuli za uchimbaji madini.

Aliongeza kuwa wakati wa kutekeleza mradi huo walibaini vikwazo mbalimbali vinavyosababisha baadhi ya waathirika kuacha kutumia dawa za kufubaza kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo za uzalishaji mali.

Kutokana na hali hiyo waliamua kutoa baiskeli kwa watu hao waliokuwa mstari wa mbele kutumia dawa hizo kikamilifu ili kuwafikia wenza ambao wameacha kutumia dawa.

"Tunafanya hivi kama kliniki inayotembea kumsaidia mtu aliyepatikana na maambukizi ya VVU kutumia dawa ili kujiweka kwenye mazingira ya kutoambukiza wengine na tukiunga mkono jitihada za serikali za kufikia 95 tatu ifikapo mwaka 2030," alisema Dk. Mwilawi.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka waganga wakuu wa wilaya kushirikiana na Shirika la HJFMRI kuweka utaratibu wa kufanya mikutano kwenye kila kijiji na kata kupata idadi kamili ya watu wanaotumia dawa za kufubaza makali ya VVU na wale walioacha ili kujua namna bora ya kuwafikia.

# Jeshi la Polisi Mbeya lapanda miti 428 kambi ya FFU

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya limepanda miti 428 kuzunguka eneo la Kambi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) mkoani Mbeya.

Hatua hiyo inaunga mkono jitihada za serikali kupanda miti ili kulinda vyanzo vya maji na kulinda mazingira.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya ambaye ni Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamini Kuzaga, jana aliongoza maofisa, wakaguzi na askari mbalimbali ya jeshi hilo kupanda miti.

"Katika kazi hii jumla ya miche ya miti 428 imepandwa kuzunguka maeneo hayo lengo likiwa ni kuunga mkono juhudi za utunzaji na uhifadhi wa mazingira," alisema ACP Kuzaga.

Kamanda Kuzaga aliwataka maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali kuendelea kuilinda na kuitunza miti hiyo ili ikue kwa ajili ya utunzaji na kupendezesha mazingira.

Aidha, alizishauri taasisi zingine kuiga mfano huo wa kupanda miti kuzunguka maeneo yao ili kuweka mazingira safi na kusaidia kukabiliana na tatizo la ukame au uhaba wa mvua.

Alisema polisi wameweka utaratibu wa kupanda miti mara kwa mara na kwamba wataendelea kufanya hivyo kama sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao.

Hivi karibuni Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania TFS , Wilaya ya Mbeya ilitoa taarifa kwa umma kuwa wanayo miche ya kutosha kwa ajili ya kuzipatia taasisi na mashirika mbalimbali zinazohitaji kupanda miche ya aina mbalimbali kama vile ya miti na matunda.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa miche hiyo inatolewa bure hivyo yoyote anayehitaji miche hiyo akifike kwenye ofisi za TFS Wilaya ya Mbeya zilizoko eneo la Airport ya zamani kupatiwa miche hiyo.

# UVCCM yalia kiwango kiduchu mikopo ya h'shauri

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, kimeiomba serikali kuongeza kiwango cha fedha za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwezesha vikundi hivyo kuendesha miradi mikubwa ya kimaendeleo na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa UVCCM, Wilaya ya Chunya, Leckson Mwakasuluka, alitoa kauli hiyo juzi walipofanya kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na utendaji kazi wake katika kuliletea maendeleo taifa.

Alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi mwitikio umekuwa mkubwa hali inayosababisha mahitaji kuongezeka.

Alisema wananchi wengi wamejiingiza kwenye shughuli za uzalishaji mali na kujiunga kwenye vikundi na kuibua uhitaji wa mikopo mikubwa kwa ajili ya kuendesha miradi yao.

"Tunaishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kutoa mikopo kwa wananchi hii imesaidia wananchi wengi kujiajiri na kuajiriwa, lakini kwa sasa mikopo inayotolewa haikidhi mahitaji yao tunaomba kiwango cha fedha kiongezeke ili wanaokopa wafanye miradi mikubwa yenye faida," alisema Mwakasuluka.

Alisema wajasirimali wanahitaji kupatiwa mitaji mikubwa ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa wanazozalisha kuliko ilivyo sasa ambapo hupata kiasi kidogo.

Baadhi ya wajasiriamali wilayani Chunya waliishukuru serikali kwa kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba ambayo imewasaidia kukuza na kuboresha biashara zao.

Agatha Mwakyoma muuzaji wa mboga na matunda alisema mkopo aliopewa umemsaidia kukuza biashara yake kutoka kuzungusha mtaani mpaka kufungua genge.

Alisema licha ya kuanzisha genge lakini bado ana ndoto ya kumiliki biashara kubwa ya mboga na matunda ambayo inahitaji mtaji mkubwa ili kufanikisha.

Alisema mpaka sasa kwenye kikundi chake cha watu saba walipatiwa Shilingi milioni nne kiasi ambacho hakitoshi.

Hivyo aliiomba serikali kufanya tathmini ya utoaji wa mikopo ili iwasaidie kutimiza malengo yao.





Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Bunge na Uratibu), George Simbachawene, akifungua kitambaa kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi katika kituo cha afya cha mama na mtoto kilichojengwa na TASAF Wilaya ya Kati Unguja. Ikiwa ni shamra shamra za Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DK. Mwinyi ajivunia mabadiliko sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali anayoiongoza imefanya mabadiliko makubwa katika sekta ya afya ili kurejesha imani ya wananchi kwa serikali yao.

Alisema kwa sasa hakuna mwananchi atakayefika kwenye hospitali ya umma akakosa dawa au vipimo, kwamba serikali imeboresha huduma za kisasa za afya na zinapatikana wakati wote.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua Hospitali ya Wilaya Kitogani, Mkoa wa Kusini Unguja ikiwa ni shamrashara za Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliitaka Wizara ya Afya kuweka maduka binafsi ya dawa kwenye hospitali zote za umma ili kuwaondolea wananchi matatizo ya kukosa dawa katika hospitali.

Dk. Mwinyi pia aliitaka wizara hiyo kuweka bajeti ya kutosha na kuwalipa kwa wakati ili kuepusha malalamiko kwa watoa huduma hizo.

Alisema kufanya hivyo ni kuondoa dhana na malalamiko ya wananchi kwamba hospitali za serikali hazina dawa na badala yake wagonjwa kutakiwa wakanunue dawa katika maduka binafsi.

Aidha, alisema Hospitali ya Kitogani ni mfano halisi wa hospitali anazozitaka kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Unguja na Pemba ili waendane na hadhi ya miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumzia dhana ya kushirikana na taasisi binafsi katika kutoa huduma za afya, Dk. Mwinyi alisema siyo kila jambo lazima lifanywe na serikali na badala yake sekta binafsi zitasimama kuwahudumia wananchi ikiwamo huduma za maabara na vipimo kama X - ray, Ultrasound na BCG.

Alisema ndani ya hospitali hiyo kuna taasisi binafsi iliyoingia mkataba na serikali wa kutoa huduma zote za vipimo vitakavyohitajika kuwatibu wananchi na kueleza tayari wameweka vifaa vyao kwa ajili ya kutoa huduma.

Alisema kwa ushirikiano huo hakuna mwananchi atakayefika hospitalini hapo na kukuta kifaa kibovu, kwamba huduma zote za kisasa zitapatikana hospitalini hapo.

"Nawataka watendaji wa Wizara ya Afya pamoja na madaktari mhakikishe mnatoa huduma bora zinazoendana na hadhi ya hospitali hii," alisema Dk. Mwinyi.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmeid Mazrui, aliwataka viongozi wa Paje kujenga kituo cha daladala kando ya hospitali hiyo ili wagonjwa na wananchi wanaofika hospitalini hapo kuwa na sehemu ya kupumzika wakati wakisubiri usafiri.

Alisema: "Nawapa muda wa wiki mbili tu viongozi wa jimbo hili ambao wanatoka CCM kujenga kituo cha daladala ili kuwaondolea usumbufu wananchi, kama hamjajenga nitakijenga mimi na mimi natokea Chama cha ACT- Wazalendo hivyo kazi kwenu," alisema Mazrui.

Mkurugenzi Mkuu kutoka Wizara ya Afya, Amour Suleiman Muhammed, alisema hospitali hiyo inauwezo wa kulaza wagonjwa 100 kwa wakati mmoja na kuhudumia wananchi 52,850.

Alisema hospitali hiyo inatoa huduma za wagonjwa wa nje, huduma za mama na mtoto, kilininiki ya pua, koo na masikio, magonjwa yasioambukiza ikiwamo kisukari, shinikizo la damu, huduma za dawa, ushauri nasaha na huduma za uchunguzi wa maabara na vipimo.

Mkurugenzi huyo alisema hospitali hiyo itaondoa msongamano kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja na wagonjwa kutoka Hospitali ya Makunduchi na maeneo jirani ya mkoa huo watahudumiwa na hospitali hapo.

# Wajasiriamali wajane watakiwa kuchangamkia mikopo nafuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wanawake ambao ni wajane wametakiwa kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali ya mikopo nafuu kwa ajili ya kufanya shughuli zao za uzalishaji mali na kupambana na umaskini.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, wakati akikabidhi vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya ujasiriamali yaliyotayarishwa na Taasisi ya Asaalam kutoka Uturuki.

Alisema katika fedha za UVIKO- 19 serikali ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni 42 kwa ajili ya wajasiriamali ambao wamegaiwa katika makundi tofauti ikiwamo wakulima wa mazao ya baharini.

Alisema katika fedha hizo wapo wakulima wa mazao ya baharini ikiwamo mwani, wafugaji wa matango bahari pamoja na kaa na samaki, kwamba Sh.bilioni 32 zimetengwa kwa kundi hilo.

Alisema ni wakati muafaka kwa wajasiriamali wanawake kuzichangamkia fedha hizo kwa malengo yaliyowekwa ya kupambana na umaskini na kuondokana na utegemezi kutoka kwa wanaume.

Aidha, alisema katika fedha hizo zipo Sh.milioni 135 ambazo zimetengwa kwa ajili ya wajasiriamali wanawake wanaojishughulisha na kazi za ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa asali.

"Wajasiriamali wanawake changamkieni fursa ambazo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwanyanyua wafanyabiashara na kuondokana na umaskini kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha za UVIKO-19 ambazo zipo," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake Wajane Zanzibar, Tabia Makame, alisema mafunzo hayo ambayo yamewahusisha wanawake wajane lengo lake kuwawezesha kushiriki katika miradi ambayo itabadilisha maisha yao kuwa bora.

Alisema hakuna sababu za kuwafanya wanawake wajane kuwa na simanzi ya kuachwa na waume zao ambapo wanatakiwa kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali katika kuwakomboa kiuchumi na maendeleo.

Meneja wa Taasisi ya Asalaam, Sadiki Mohamed Ali, alisema mafunzo hayo yamelenga katika kuongeza ubunifu kwa wanawake katika uzalishaji wa mali na bidhaa mbalimbali ili kuingia katika ushindani wa soko.

Alisema Taasisi ya Asalaam inatoa elimu ya ujasiriamali ambayo huwawezesha wahitimu wake kuingia katika ushindani wa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa mafanikio makubwa.

# ZRB yatakiwa kuandaa mifumo ya kielektroniki kuongeza mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ameutaka uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kuandaa mifumo madhubuti ya kielektroniki ambayo itasaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mkutano wa kutathmini utendaji kazi wa ZRB kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba 2022.

Alisema serikali inahitaji mapato kwa kuendesha miradi ya maendeleo pamoja na kukuza uchumi wake hivyo uwepo wa mifumo madhubuti itasaidia kukuza ukusanyaji huo kwa maslahi ya taifa.

Aliipongeza ZRB kwa mafanikio yanayoendelea kupatikana ambayo ni ya kuridhisha na kusisitiza juhudi zaidi na uwajibikaji wa pamoja unahitajika ili kuimarisha wigo wa ukusanyaji wa mapato.

Hemed alisema kuwa watendaji wa ZRB wana wajibu wa kusimamia sheria na taratibu zilizoko ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Alisema ukusanyaji wa mapato unahitaji nidhamu kwa kuheshimu fedha za serikali na kuwataka watendaji hao kuwa waaminifu na wazalendo kwa taifa.

Aidha, aliwataka watendaji hao kuwaelimisha na kuwasimamia walipa kodi na kuacha muhali ili kulipa kodi kwa mujibu wa sheria na suala la ulipaji wa kodi siyo la kujuana bali ni la kisheria.

Hata hivyo alisema serikali inaamini katika dhana ya tozo ndogo kwa walipakodi ili kila mfanyabiashara na mwananchi anayepaswa kulipa kodi kulipa kikamilifu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema kuwa mafanikio yaliyopatikana katika bodi hiyo yamefikiwa kutokana na maelekezo ya viongozi wakuu wa serikali na kuahidi kuendelea kusimamia maelekezo wanayopatiwa ili kufikia dhamira ya Rais Dk. Mwinyi ya kujenga Zanzibar mpya.

Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar, Yusuph Juma Mwenda, alisema mkutano huo una lengo la kujitathmini kipindi cha robo mwaka pamoja kuandaa mikakati madhubuti ya kuendeleza bodi hiyo.

Aidha, alisema kuwa lengo la ZRB ni kuwa karibu na walipa kodi na kufanya suala la ulipaji wa kodi uwe rahisi ili kufikia lengo la ukusanyaji.




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta (kushoto), mwishoni mwaka wiki alipokea msaada wa baiskeli 20 kutoka Shirika la HJF Medical Research International (HJFMRI) zilizotolewa na Dk. Emmanuel Bahemana (kulia), kwa niaba ya Mkurugenzi wa shirika hilo kwa ajili ya kuwapatia mawakili tiba wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVVU) kwa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Hizi ni sababu za ugonjwa afya ya akili

**Na Elias Sabuni**

SASA hivi kuna usemi unaotumika katika simulizi watu wanasema "Ukubwa ni Dawa". Mimi katika hili nawaunga mkono hao wanaosema hivyo maana wahenga wanasema: "Kuishi kwingi ni kujua/kuona mengi".

Katika hali ya kusikitisha, Watanzania sasa tumejikuta katika tatizo la ugonjwa wa akili. Enzi za Wahenga ugonjwa huu ulijulikana kuwa ni ugonjwa wa kurithi, sasa hivi sio hivyo tena. Taasisi moja iliyoko hapa nchini inayojulikana kwa jina la Tap Elderily Women's Wisdom for Youth (TEWWY), inayofanya kazi ya kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kujiepusha na tatizo la ugonjwa wa akili inasema tatizo la ugonjwa wa akili linaongezeka mwaka hadi mwaka.

TEWWY inatumia mtandao wa jamii unaosukumwa na mahitaji na uwajibikaji kwa kutoa unasihi kwa mtu binafsi, ushauri katika vikundi na stadi za maisha katika kujijali, stadi za kazi na ujasiriamali na jinsi ya kuhitimu mihemuko na masuala ya elimu ya afya na uzazi. Matukio ya mauaji yanayotokea nchini yameleta hofu kubwa kwa wazee wastaafu nchini ambao hawaelewi kama mauaji yanatokea nchini ni ya makusudi ama ni bahati mbaya. Hofu ya Wahenga hawa inapata jibu kutokana na Shirika la Afya Duniani (WHO) linalosema kwamba ifikapo mwaka 2030 sonona itachangia ongezeko kubwa la ugonjwa wa akili duniani (WHO 2005).

Wale wenye kumbukumbu nzuri watakumbuka kuwa tangu tupate uhuru nchi yetu imekuwa na hospitali moja tu mkoani Dodoma ambayo ni maalumu kwa ajili ya kutoa huduma kwa tiba ya wagonjwa wa akili. Mkurugenzi wa Afya ya Akili Hospitali ya Mirembe, Dk. Paul Lawala, katika kubainisha tatizo la ugonjwa huu anasema; nchi ina wagonjwa kati ya 6,000 hadi 7,000.

Shirika la Afya Duniani, mwaka 2005 lilitoa taarifa inayosema mazingira duni ya kijamii na kiuchumi, unyanyapaa, upuuzaji na uvujifu wa haki za binadamu vyote huchangia matatizo ya afya ya akili. Ugonjwa wa akili kama sio wa kuzaliwa nao, mtu anaweza kufikwa na tatizo hili kutokana na mazingira ya watu wanaomzunguka, kipato cha mahitaji, mapenzi na kwa vijana ni malezi anayopata kutoka kwa wazazi. Hali nyingine inayodaiwa kusababisha tatizo la akili ni ugovi wa mara kwa mara na ndoa.

TEWWY katika dhamira yake ya kupambana na tatizo hili la akili inaamini katika uwezo wa kinamama na watu wazima katika kuchangia masuala ya afya ya akili kwa kutumia hadithi, simulizi, subira na uwezo wa kusikiliza na imani ya vijana kwao hasa katika masuala ya afya ya wazazi.

Ugonjwa wa akili tiba yake ni nzito mno. Nakumbuka kuna ndugu yangu kitendo cha ukatili cha kutaka kumuua ndugu yake; lakini alipofikishwa polisi, alionyesha vitendo vya mtu anayechanganyikiwa, polisi walimpeleka Hospitali ya Mirembe huko Dodoma ambako alikaa mwaka na miezi saba ndipo alipoonekana amepona.

Daktari Bingwa wa Afya ya Akili katika hospitali hiyo akiongea na mwanahabari amesema kuwa tiba ya ugonjwa wa akili inafikia hadi miaka mitatu mtu kupona. Vijana wengi wanafanya uhalifu mitaani na kuonyesha dalili za kuchanganyikiwa; hupelekwa kituo cha Isanga na baadaye Hospitali ya Mirembe. Hao ndio Dk. Sadik Mandari anasema, huchukua hadi miaka mitatu kupona.

TEWWY wanadai kuwa wakiunganisha uzoefu katika maisha na stadi za maisha ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali; kupitia hadhira za afya ya akili na stadi za maisha tatizo la ugonjwa wa akili linaweza kupotea kabisa. Vitendo vya watu kujiua (suicide) hivi sasa vimezidi kuongozeka duniani; kuanzia vijana wa miaka 10-34 na limekuwa ni tukio la nne katika kusababisha vifo kwa vijana na wazee kati ya miaka 35 hadi 44. Kiasi cha watu 850,000 hufa kwa kujiua kila mwaka duniani ambayo ni sawa na mtu mmoja kila sekunde 40. Kutokana na hali hiyo mtu unaweza kusema ugonjwa wa akili ni silaha inayohitaji kuondolewa katika maisha ya binadamu.

***Email: eliassabuni22300@gmail.com.***

# Mwasa ampongeza Samia kuidhinisha bil. 267/- za maji

**Na Christina Haule, ULANGA**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha Sh. bilioni 267 kuingia kwenye miradi ya maji mkoani hapo na kutengeneza historia tangu nchi kupata uhuru kwa kuhakikisha hakuna kero mkoa mzima.

Mwasa alitoa pongezi hizo jana mbele ya Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Kituti kilichoko Tarafa ya Ruaha, wilayani Ulanga mkoani hapo na kumshukuru kuwa waziri wa kwanza kupita kijiji kwa kijiji kutatua kero za maji kwa vitendo.

Akitoa mchanganuo wa fedha hizo, Mwasa alisema Sh. bilioni 185 ni kwa ajili ya kuboresha Bwawa la Mindu na kusambaza mtandao wa maji ili kuondoa tatizo Morogoro Mjini ambako maji yanayotumiwa ni zaidi ya asilimia 85.

"Ni dhahiri kuwa kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kukomesha changamoto ya maji kwa Morogoro Mjini kwa zaidi ya miaka 50 ijayo na kuhakikisha hakuna mtu atakayelalamika kukosa maji," alisema.

Alisema Sh. bilioni 17 kati ya hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi midogo midogo ya usambazaji wa maji mijini, kazi inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 80.

Mwasa alisema kwa maji vijijini, Rais ametoa Sh. bilioni 65 zinazotekeleza miradi vijijini ikiwamo uzinduzi wa mradi wa maji wa Sh. milioni 266 katika Kijiji cha Kituti, Tarafa ya Ruaha, wilayani Ulanga mkoani hapa ambako maji yanatoka na mradi unaendelea.

"Samia haongei mengi ila anatenda mengi ametenda, ameweza na kuzidi, hongera nyingi sana kwake, lakini Waziri Aweso asipoombwa anatoa ila akiombwa anatoa zaidi, haya mabilioni mengi niliyoyasema mimi hatukuwa tumeomba, lakini yamekuja," alisema Mwasa.

Akizungumzia mradi wa maji Kituti, uliogharimu Sh. milioni 299, Waziri Aweso alisisitiza wananchi, kamati na jumuiya za watumiaji maji kusimamia vyema miradi ya maji iliyowekwa na kuhakikisha inadumu kwa wananchi kuchangia ukarabati wa miundombinu kwa kulipia ada kama inavyopaswa.

Meneja wa Maji kutoka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Ulanga, Injinia David Kaijage, alisema mradi wa maji Kituti uliofikia asilimia 92 mpaka sasa utahudumia wakazi 2,692 ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inayosema watu wapate maji maeneo wanayofikika.

Lawi alisema katika miradi inayotekelezwa kwenye wilaya hiyo mpaka sasa wana asilimia 71 kwa vijijini na 75 mjini kwa matumizi ya maji.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kituti, Siliva Lyanhera, alimshkuru Rais Samia kwa hatua ya kuwasaidia kupata majisafi na salama na kwamba alipo mama wanaKituti wapo.

"Wananchi wangu wa Kituti kwa sasa watapata majisafi na salama na kuondokana na maji ya mito, hayajapimwa, hayana dawa ni Mungu tu ndio anatulinda hatuumwi umwi, sasa tunashukuru kwa kweli," alisema Lyanhera.

## HABARI KIMATAIFA

# M23 wakabidhi kambi ya jeshi Rumangabo

**KINSHASA, DRC**

WAASI wa M23 wameirudisha kambi ya kijeshi ya mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRD) katika hatua ya kutimiza ahadi yake ya kuondoka kwenye maeneo waliyoyanyakua na kuyadhibiti kwa miezi kadhaa.

Wakazi wa eneo hilo la mashariki ya Kongo Ijumaa walielezea furaha yao wakati waasi hao walipokabidhi vifaa na kambi ya kijeshi ya Rumangabo, kubwa zaidi katika eneo la mashariki mwa mkoa wa Kivu Kaskazini, licha ya kudai kwamba bado wametawaliwa na wasiwasi.

Hafla ya kukabidhi kambi hiyo ya Rumangabo kwa vikosi vya kulinda amani vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF) inaashiria mwanzo wa kuondoka kwa wapiganaji wa kundi la M23 kutoka kwenye mji wa kimkakati wa kijeshi wa Rumangabo, ulio kilomita 40 kaskazini mwa mji mkuu wa mkoa wa Goma, ambao waasi waliuteka mwishoni mwa Oktoba 2022.

Kwa mujibu wa waandishi wa habari wa shirika la AFP walioruhusiwa kuripoti juu ya makabidhiano hayo, shughuli hiyo ilisimamiwa na vikosi vya Kenya vya kulinda amani vilivyopelekwa nchini Kongo na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba shughuli hiyo ya jana inafuatia makabidhiano kama hayo ya mwezi uliopita ya kambi ya Kibumba, iliyo karibu kilomita 20 kusini mwa Kongo.

Jenerali Emmanuel Kaputa Kasenga, naibu kamanda wa kikosi cha Afrika Mashariki alisema kudhibiti tena kambi ya Rumangabo kunaashiria hatua muhimu katika juhudi zinazoendelea za kuleta amani na utulivu katika eneo la mashariki nchini DRC.

Naibu kamanda huyo alisema vikosi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vitaendelea kusimamia utaratibu wa kurudishwa maeneo yaliyotekwa na waasi wa M23 na ameyataka makundi mengine kufuata utaratibu huo na kusalimisha silaha zao.

Kiongozi wa M23, Imani Nzenze, alisema katika hafla hiyo ya kwamba wao wanataka amani na wataendelea kujumuika katika mchakato huo wa kutafuta amani na ndio sababu kundi lake la M23 limeamua kukabidhi rasmi kambi ya kijeshi ya Rumangabo kwa kikosi hicho cha Afrika Mashariki.

Viongozi wa kikanda walifanikisha kufikiwa makubaliano kati ya pande hasimu Novemba 2022 hatua inayolifanya kundi la M23 kuondoka na kukabidhi maeneo waliyoyanyakua, hatua itakayowawezesha watu waliogeuka wakimbizi wa ndani kurejea katika makazi yao waliyoyakimbia.

***DW***



Waasi wa M23 wakilinda wakati wa hafla ya makabidhiano ya kambi ya Rumangabo. **PICHA: DW**

# Ukraine yapokea silaha za kujikinga na makombora

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine, Volodymr Zelenskyy, amepongeza msaada wa silaha kutoka Marekani, unaojumuisha magari yenye uwezo wa kurusha makombora ya kuharibu vifaru vya kivita.

Zelenskyy alisema kwamba msaada huo uliotolewa na Marekani wa mabilioni ya dola ndio unaohitajika kwa Ukraine ambayo inaendelea kupambana na wanajeshi wa Russia, huku ikibainishwa kuwa msaada huo wa kijeshi wa hivi punde kwa Ukraine ndio mkubwa zaidi kuwahi kutolewa.

Katika hotuba ambayo imepeperushwa mara kadhaa na vyombo vya habari nchini Ukraine, Rais Zelenskyy ameutaja msaada wa Marekani kuwa wenye nguvu sana.

Ukraine ilisema kwamba tangazo la kusitisha vita lililotolewa na Russia kwa ajili ya krismasi ya Orthodox, limekiukwa na baadhi ya wanajeshi wake wanaoendelea kupigana wakati vita hivyo vinaingia mwezi wa 11.

Gavana wa mji wa Sevastopol, ambaye aliteuliwa na Russia baada ya kuudhibiti mji huo kutoka kwa Ukraine, aliandika ujumbe wa Telegram akisema kwamba wanajeshi wa Russia wameangusha ndege isiyokuwa na rubani, iliyokuwa inalenga kuushambulia mji huo.

Ukraine ilisema kwamba ina lengo la kurejesha sehemu zote ambazo zilichukuliwa na Russia zikiwamo zilizochukuliwa kabla ya uvamizi wa sasa, ikiwamo Crimea iliyonyakuliwa mwaka 2014.

Rais wa Russia, Vladimir Putin, alihudhuria misa ya kusherehekea krismasi ya Orthodox katika kanisa kuu la Kremlin na alikuwa muumini pekee katika misa hiyo iliyofanyika usiku.

Aidha, inaelezwa kuwa Kanisa la Orthodox nchini Russia linaunga mkono uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

***VOA***

## Waandishi 6 kizuizini madai kumwaibisha Rais

**JUBA, Sudan Kusini**

MASHIRIKA ya kutetea haki za vyombo vya habari yanasema waandishi wa habari sita nchini Sudan Kusini wamekamatwa kutokana na kusambaa kwa picha za video zinazomwonyesha Rais Salva Kiir akitokwa na haja ndogo.

Desemba 2022, kulisambaa video kwenye mitandao ya kijamii iliyoonekana ikimwonyesha Rais Kiir akijikojolea huku wimbo wa taifa ukipigwa kwenye hafla.

Inaelezwa kuwa wafanyakazi sita kutoka shirika la utangazaji la serikali walikamatwa wiki hii, huku kamati ya kulinda wanahabari (CPJ) ikishinikiza waachiliwe.

Patrick Oyet, Rais wa Muungano wa waandishi wa habari wa Sudan Kusini, aliambia Reuters kwamba waandishi hao wanashukiwa kufahamu kuwa video hiyo ilivujaje.

Shirika la Utangazaji la Sudan Kusini (SSBC) linasema video hiyo haikuonyeshwa kwenye kituo hicho.

Waziri wa Habari wa Sudan Kusini, Michael Makuei, aliiambia Sauti ya Amerika kwamba watu wanapaswa kusubiri kujua kwa nini wanahabari hao walikamatwa.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu mara kwa mara yametaka mamlaka za Sudan Kusini kuacha kuwanyanyasa na kuwatishia waandishi wa habari.

***BBC***

## EU yakosoa hukumu kifo kwa waandamanaji Iran

**TEHRAN, Iran**

MSEMAJI Mkuu wa Sera za Mambo ya Nje wa Umoja wa Ulaya (EU), Josep Borrell, amesema wanashangazwa na uamuzi wa Iran kwa Mohammad Karami na Seyyed Hussein, waliokamatwa na kuhukumiwa kifo kutokana na maandamano yanayoendelea nchini Iran.

EU ambao inashutumu ishara mpya ya ukandamizaji wa maandamano, kwa mara nyingine tena inatoa wito kwa mamlaka ya Iran kukomesha mara moja tabia inayolaumiwa ya kutamka na kutekeleza hukumu za kifo dhidi ya waandamanaji. Pia EU ilitaka Iran kufuta haraka hukumu za kifo za hivi karibuni ambazo tayari zimetolewa katika muktadha wa maandamano.

Shirika la habari la vyombo vya sheria Mizan Online, lilitangaza kuwa wanaume wawili walinyongwa juzi, nchini Iran baada ya kupatikana na hatia na mahakama ya Iran ya kumuua mwanajeshi wakati wa maandamano yaliyosababishwa na kifo cha kijana mmoja Mkurdi aliyepatikana amefariki dunia akiwa gerezani.

Vijana wawili walionyongwa Jumamosi hii asubuhi ni Mohammad Mehdi Karami na Mohammad Hosseini, ambao walishtakiwa pamoja na watu wengine 14 kwa mauaji ya mwanamgambo wa Kiislamu Novemba 2022 wakati wa maandamano ya kupinga mamlaka.

***RFI***

# MABONDIA 18 KUZIPIGA USIKU WA KIDUNDA, MKONGOMANI

**Na Saada Akida, Zanzibar**

JUMLA ya mabondia 18 wanatarajiwa kupanda ulingoni Februari 24, mwaka huu, kusindikiza pambano la kimataifa la Ubingwa wa ABU kati ya Mtanzania Selemani Kidunda na Patrick Mukala wa DR Congo.

Kidunda atapanda ulingoni katika pambano hilo ikiwa ni baada ya kupita miezi sita tangu alipomchapa kwa pointi Tshimanga Katompa kutoka DR Congo Julai mwaka jana, katika pambano la kuwania Ubingwa wa Dunia wa WBF ambalo lilipigwa Songea mkoani Ruvuma.


Akizungumza na gazeti hili jana, promota wa pambano hilo kutoka Kemmon Sports Agency, Sada Kasonso, alisema Kidunda na Mukala watapanda ulingoni kwenye pambano hilo la kuwania mkanda wa Ubingwa wa ABU huku kukiwa na mapambano mengine tisa ya utangulizi yatakayokuwa na mabondia 18.

"Ni kweli Kemmon Sports Agency ndiyo waandaaji wa pambano kubwa la kimataifa litakalowakutanisha Mtanzania, Kidunda dhidi ya Patrick (Mukala) kutoka DR Congo ambaye makazi yake ni Afrika Kusini.

"Mabondia wote tayari wameshasaini mikataba na sasa wameanza maandalizi kwa ajili ya pambano hilo ambalo tunategemea litakuwa na upinzani mkali," alisema na kuongeza;

"Lakini ukiondoa pambano hilo ambalo litakuwa ndilo kubwa, tutakuwa na mapambano mengi ya utangulizi ambayo yatawakutanisha mabondia 18 katika mapambano tisa ambayo yote yatakuwa makali kutokana na aina ya mabondia watakaopanda ulingoni siku hiyo ingawa kwa sasa kama waandaaji tunakaribisha wadhamini ili kuweza kutoa sapoti."

**TUMEWASILI...**




Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu (katikati), akipozi katika picha na wachezaji wake, Pape Sakho (kushoto) na Peter Banda, baada ya timu hiyo kutua Dubai juzi usiku kwa kambi ya wiki moja kujiandaa na michuano ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika. Banda amerejea rasmi kikosini baada ya kuwa nje akiuguza majeraha ya mguu. **PICHA: SIMBA**

# Namungo yataka Kombe Mapinduzi

**Na Saada Akida, Zanzibar**

NUSU fainali ya pili ya Kombe la Mapinduzi itapigwa leo katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar ikiwakutanisha Namungo FC dhidi ya Mlandege.

Mchezo huo utapigwa saa 2:15 usiku na mshindi wa mechi hiyo atakutana fainali na timu iliyoshinda nusu fainali ya kwanza jana usiku kati ya Azam FC na Singida Big Stars.

Namungo FC wameingia hatua ya nusu fainali baada ya kufanikiwa kupata pointi nne kutoka Kundi D, lililokuwa likijumuisha timu za Chipukizi ya Zanzibar na Aigle Noir ya Burundi.

Katika kundi hilo Namungo ilifuzu nusu fainali baada ya mchezo wa kwanza kutoka suluhu dhidi ya Chipukizi na kuibuka na ushindi mchezo wa pili dhidi ya Aigle Noir.

Kuelekea mchezo huo Kocha wa Namungo FC, Denis Kitambi, amesema wamefanya maandalizi mazuri na wachezaji wapo tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo huo.

Alisema mechi itakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu amewaona Mlandege FC ni timu ngumu na nzuri, lakini wako tayari kuhakikisha wanafikia malengo yao.

"Tumekuja katika mashindano haya kwa malengo yetu ikiwamo kufika nusu fainali na sasa tunahitaji kucheza fainali, ili kufika hapo lazima tuwaheshimu wapinzani wetu na kucheza kwa tahadhari kubwa kutafuta ushindi dhidi ya Mlandege," alisema Kitambi.

Alisema mashindano hayo yamemsaidia kupata mwanga wa kikosi chake hasa kwa wachezaji wapya ambao amewapa nafasi kwa ajili ya kutengeneza muunganiko wa nyota hao na wazamani.

# Opa ampiku Mkenya mabao Ligi ya Wanawake

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Timu ya Soka ya Wanawake ya Simba Queens, Opa Clement, kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu hiyo baada ya kufikisha mabao manne akimpiku mchezaji wa Fountain Gate Princess, Cynthia Musungu raia wa Kenya ambaye amesalia na matatu.

Opa alifungia Simba Queens bao dhidi ya Fountain Gate Princess kwenye ushindi wa mabao 2-1 Jumatano iliyopita katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kufikisha idadi hiyo ya mabao.

Kabla ya mechi hiyo, Opa na Cynthia wote walikuwa na mabao matatu kila mmoja kwenye mechi tatu ambazo timu zao zimecheza, lakini timu hizo zikakutana zenyewe kwenye mechi ya raundi ya nne na mshambuliaji huyo wa Simba akafunga bao huku mwenzake akishindwa kuweka mpira wavuni hadi dakika 90 za mchezo zinamalizika.

Straika huyo amefunga mabao manne kwenye mechi nne ambazo timu yake imecheza.

Hakuna mchezaji mwingine aliyefikia idadi hiyo ya mabao kwenye mechi zilizofuata za ligi hiyo.

Kwenye mechi zingine zilizofuata Alhamisi iliyopita, Mkwawa Queens ilichapwa nyumbani, Uwanja wa Samora, Iringa bao 1-0 dhidi ya Amani Queens na Ijumaa kwenye uwanja huo huo, Ceasiaa Queens nayo ilipata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya JKT Tanzania.

Ligi hiyo imefika raundi ya nne, JKT Queens ikiongoza kwa pointi 10, huku Fountain Gate Princess baada ya kufungwa na Simba ikishuka hadi nafasi ya pili ikiwa na pointi tisa, Yanga Princess baada ya kuitungua Alliance Girls mabao 5-2 Jumamosi, ipo nafasi ya tatu kwa pointi saba, na Simba Queens ina pointi saba kwenye nafasi ya nne, wakati Yanga Princess ikikaa juu kwa idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

## ZISIKUPITE

### FELIX AWINDWA ZAIDI

KLABU ya Atletico Madrid inataka pauni milioni 9.5 kama ada ya mkopo na kipengele cha kununuliwa kwa pauni milioni 70 kutoka Manchester United wakati majadiliano yakiendelea kuhusu fowadi wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23. ***(Sunday Mirror)***

### MARTINEZ KUINOA URENO

KOCHA wa zamani wa Everton, Roberto Martinez, ambaye alikuwa kocha wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji kwa miaka sita kabla ya kujiuzulu mwaka jana, amefikia makubaliano ya kuinoa Ureno.***(Athletic)***

### PICKFORD ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamwania golikipa wa Everton na England, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 28, kuch***ukua nafasi ya nahodha wa Ufaransa, Hugo Lloris, 36. (Sunday Mirror)***

### ABOUBAKAR ANUKIA UNITED

KLABU ya Al-Nassr imemwachia straika wa Cameroon, Vincent Aboubakar, mwenye umri wa miaka 30, ambaye amekuwa akihuishwa na kutua Manchester United kuziba nafasi ya Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37***. (Al-Riyadh)***

### INGS ATAJWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace ipo tayari kushindana na Everton katika mbio za kumsajili straika wa zamani wa England, Danny Ings mwenye umri wa miaka 30 kutoka Aston Villa. ***(Sun)***

### ZERBI AMSHTUA TROSSARD

KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi, amemwambia Leandro Trossard, anataka zaidi kutoka kwake***. (The Athletic)***

### BARBER AZIONYA CHELSEA, LIVER

OFISA Mtendaji wa Brighton, Paul Barber, amewaonya Chelsea na Liverpool kwamba watatakiwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha ili kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21. ***(Metro)***

### THURAM KUTUA CHELSEA

CHELSEA imefungua mazungumzo na Borussia Monchengladbach kuhusu usajili wa mchezaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, Marcus Thuram ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### RUTTER KUTUA LEEDS

LEEDS United inataka kumsajili fowadi wa Hoffenheim, Georginio Rutter, mwenye umri wa miaka 20. ***(Sky Sports Germany)***

### MUDRYK AWEKEWA NGUMU

WAKALA wa Ukraine, Igor Kryvenko, anaamini Shakhtar Donetsk hawatamwachia winga, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 22, kuondoka klabuni hapo licha ya kumsusishwa na Arsenal. ***(Footboom via FourFourTwo.com)***



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE AKATAA KUWA KOCHA WA MAREKANI

●●●Mshindi huyo mara tatu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, pia amekuwa akihusishwa na Timu za Taifa za Brazil na Ureno lakini...

**PARIS, Ufaransa**

ZINEDINE Zidane amekataa ombi la Shirikisho la Soka la Marekani kuchukua nafasi ya Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanaume, kwa mujibu wa ESPN.

Zidane, kupitia wakala wake, Alain Migliaccio, aliulizwa kama angependa kumrithi Gregg Berhalter, kama kocha wa Marekani, ambapo Mfaransa huyo alikataa.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia la 1998, ambaye alitimiza umri wa miaka 50 Juni mwaka jana, amekuwa hana klabu tangu mwisho wa kipindi chake cha pili cha kuinoa Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2021, lakini kuna wakati alihusishwa na Ufaransa.

Jumamosi Didier Deschamps aliongezewa mkataba wa kuinoa Timu ya Taifa ya Ufaransa hadi mwaka 2026 na hivyo kuzima uvumi wa Zidane kupewa nafasi hiyo.

Mshindi huyo mara tatu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, pia alikuwa akihuishwa na Timu za Taifa za Brazil na Ureno.

Mkataba wa Berhalter kama kocha wa Marekani ulimalizika Desemba 31, mwaka jana, huku shirikisho hilo likitangaza wiki hii kwamba Kocha Msaidizi, Anthony Hudson, atachukua jukumu la mechi ya kirafiki dhidi ya Serbia Januari 25 huko Los Angeles na dhidi ya Colombia siku tatu baadaye huko Carson, California.

Marekani itaandaa kwa pamoja Kombe la Dunia la 2026, pamoja na Canada na Mexico.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 440

MECHI KALI
OXFORD UTD
VERSUS
ARSENAL
1 | 11.26
X | 6.42
2 | 1.19

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOCHA CHELSEA HANA HOFU YA KUTIMULIWA



**LONDON, England**

KIPIGO cha sita kwa Chelsea katika Ligi Kuu England msimu huu kiliwaacha katika nafasi ya 10, lakini kocha Graham Potter, amesema anaendelea kuungwa mkono na wachezaji na wamiliki wa klabu hiyo.

Chelsea, ambayo ilitangaza kumsajili mshambuliaji wa Molde, David Datro Fofana, Jumamosi ilifanya vibaya chini ya Potter katika wiki za hivi karibuni na kipigo chao cha bao 1-0 kutoka kwa Manchester City Alhamisi kilikuwa cha nne katika mechi sita za ligi.

Klabu hiyo ya London pia ilitupwa nje ya Kombe la Ligi na City Novemba, na kuharibu matarajio yao ya kushinda taji msimu huu, ingawa bado wapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na watacheza na Borussia Dortmund katika hatua ya 16-bora.

Potter alizungumzia mwanzo wa Pep Guardiola, Jurgen Klopp na Mikel Arteta wakiwa City, Liverpool na Arsenal na ukweli kwamba watatu hao walishindwa kushinda kombe katika misimu yao ya kwanza ya kuzinoa klabu zao.

"Nadhani Pep alikuwapo mwaka mmoja kabla hawajashinda chochote, halafu ni wazi Mikel na Juergen walichukua muda kidogo," alisema Potter akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mechi ya jana Jumapili ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya City.

"Inaweza kuwa tofauti kwangu, lakini siweki mpangilio wa wakati juu yake.

"Ninajua kuwa nina uwezo na najua ubora nilionao. Ninaungwa mkono kabisa na wamiliki na wachezaji na wafanyakazi wa hapa. Na unaweza kuona kwa msaada tulionao huko nje, ni mzuri.

"Siku zote kutakuwa na watu ambao wana shaka, lakini siko hapa kumshawishi mtu yeyote. Niko hapa kufanya kazi yangu. Na ikiwa hilo litawashawishi ni sawa."

# Ten Hag asisitiza nidhamu United

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amewaambia wachezaji wake wa Manchester United kuwa ataendelea kudhibiti nidhamu ya kikosi baada ya kumwondoa Cristiano Ronaldo na kumsimamisha Marcus Rashford.

Ronaldo alisitishiwa mkataba wake baada ya kumkosoa Ten Hag na klabu katika mahojiano na Piers Morgan huku Rashford akiadhibiwa kwa kuchelewa kwenye mkutano wa timu.

Ten Hag amesema ataendelea kuweka sheria kali pale Old Trafford.

"Iwapo unataka kuendeleza kitu, ikiwa unataka kujenga mtazamo wa ushindi na utamaduni wa kushinda lazima uende hivi kwa maoni yangu," alisema Ten Hag.

"Kila mtu atafanya kwa njia yake, lakini ukimruhusu asiwe na nidhamu, ikiwa hauendani na viwango, maadili na sheria tulizowekwa kama timu na kama wafanyakazi.

"Ukiwa uwanjani hilo litafanyika ikiwa huna nidhamu inayohitajika kushinda michezo. Ni jukumu kubwa kwa hiyo lazima uende hivyo."

Ten Hag aliwaambia mabosi wa United hakuna njia ya kurudi kwa Ronaldo baada ya mahojiano yake na Morgan.

Rashford, wakati huohuo, aliwekwa benchi kwenye mchezo wa Wolves Desemba 31, mwaka jana kabla ya kuja kufunga bao katika ushindi wa 1-0.

"Ikiwa ni mtu sahihi na binadamu sahihi na tabia sahihi, watafanya hivi," alisema Ten Hag.

"Kuhusiana na Marcus, nilikuwa na hakika juu yake kwa sababu nimemfahamu kwa miezi saba au nane."



,981,840

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11.01.23 | 20:00 | AEL Limassol vs Apollon Limassol | 2.73 | 3.22 | 2.37 |
| 02. 11.01.23 | 20:00 | Kortrijk vs Mechelen | 2.62 | 3.41 | 2.44 |
| 03. 11.01.23 | 21:00 | Nantes vs Lyon | 3.22 | 3.31 | 2.19 |
| 04. 11.01.23 | 21:00 | AJ Auxerre vs Toulouse | 2.64 | 3.29 | 2.54 |
| 05. 11.01.23 | 21:00 | AC Ajaccio vs Reims | 2.90 | 3.10 | 2.46 |
| 06. 11.01.23 | 22:00 | VVV Venlo vs Emmen | 3.05 | 3.49 | 2.17 |
| 07. 11.01.23 | 22:45 | Nottingham vs Wolverhampton | 2.63 | 3.12 | 2.68 |
| 08. 12.01.23 | 02:00 | Alebrijes De Oaxaca vs Club Celaya | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 09. 12.01.23 | 04:05 | Cancun FC vs Leones Negros Udg | 2.63 | 3.07 | 2.53 |
| 10. 12.01.23 | 18:00 | Ghazl EL Mahallah vs Enppi Club | 2.65 | 2.65 | 3.15 |
| 11. 12.01.23 | 20:45 | Heracles Almelo vs GO Ahead Eagles | 2.21 | 3.51 | 2.96 |
| 12. 12.01.23 | 22:45 | Union Saint Gilloise vs KAA Gent | 2.24 | 3.45 | 3.10 |
| 13. 13.01.23 | 11:45 | Macarthur FC vs Central Coast Mariners | 2.47 | 3.28 | 2.74 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 09/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1202 | FC Vizela U23 vs Gil Vicente FC U23 | 2.06 | 3.75 | 2.87 |
| 14:00 | 1777 | Aizawl FC vs Real Kashmir | 2.15 | 3.16 | 3.16 |
| 15:20 | 3368 | AL Qaisoma vs AL Khlood | 2.54 | 2.74 | 2.93 |
| 15:30 | 4354 | Vietnam vs Indonesia | 1.56 | 3.61 | 5.47 |
| 15:40 | 3728 | Al Orubah vs Ohud Medina | 2.26 | 2.78 | 3.36 |
| 16:15 | 2217 | Oman vs Yemen | 1.38 | 3.89 | 8.37 |
| 16:15 | 5926 | PO Triglias vs Diagoras FC | 1.34 | 4.28 | 8.18 |
| 17:00 | 2331 | Basaksehir vs Adana Demirspor | 2.06 | 3.44 | 3.34 |
| 17:10 | 4463 | Jeddah Club vs Al Jabalain | 3.17 | 2.83 | 2.32 |
| 18:00 | 1300 | Panetolikos vs OFI Crete | 2.38 | 2.98 | 3.13 |
| 19:15 | 2020 | Saudi Arabia vs Iraq | 2.53 | 2.91 | 2.77 |
| 20:00 | 1488 | Aris Limassol vs Akritas Chlorakas | 1.25 | 5.56 | 10.93 |
| 20:00 | 3153 | Ironi Tiberias vs Ahi Nazareth | 1.94 | 3.45 | 3.79 |
| 20:00 | 3240 | Olympiakos Nicosia vs Karmiotissa | 2.41 | 3.36 | 2.81 |
| 20:00 | 3292 | Istanbulspor vs Gaziantep BB | 2.74 | 3.44 | 2.38 |
| 20:00 | 3868 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Petah Tikva | 2.76 | 3.16 | 2.56 |
| 20:00 | 4262 | Pachuca U20 vs Puebla U20 | 1.65 | 3.95 | 4.70 |
| 20:00 | 4476 | Alanyaspor vs Trabzonspor | 2.98 | 3.53 | 2.19 |
| 20:00 | 5928 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Afula | 2.47 | 3.19 | 2.84 |
| 20:30 | 4984 | Verona vs Cremonese | 2.04 | 3.27 | 3.52 |
| 21:15 | 2286 | Al Shabab Riyadh vs Al Ittihad Jeddah | 2.35 | 3.55 | 2.75 |
| 21:30 | 3392 | Hapoel Beer Sheva vs Hapoel Tel Aviv | 1.48 | 4.18 | 5.44 |
| 21:45 | 4588 | Sweden vs Finland | 1.77 | 3.53 | 4.74 |
| 22:00 | 2065 | Leicester U21 vs Chelsea U21 | 4.87 | 4.48 | 1.49 |
| 22:00 | 5318 | Jong Utrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.60 | 3.33 | 2.50 |
| 22:30 | 4209 | US Ancona 1905 vs Pontedera | 2.06 | 3.26 | 3.61 |
| 22:45 | 4926 | Redditch United vs Bedford Town Football Club | 1.81 | 3.90 | 3.42 |
| 22:45 | 5574 | Bologna vs Atalanta | 3.41 | 3.31 | 2.06 |
| 23:00 | 1896 | Huesca vs Albacete Balompie | 2.37 | 2.97 | 3.12 |
| 23:00 | 1933 | Oxford Utd vs Arsenal | 11.26 | 6.42 | 1.19 |
| 23:00 | 2345 | Athletic Bilbao vs Osasuna | 1.66 | 3.65 | 5.19 |
| 23:15 | 5243 | Tondela vs Penafiel | 2.36 | 3.21 | 2.86 |

### JUMANNE - 10/01/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 1856 | Humble Lions FC vs Cavaliers FC | 3.21 | 2.82 | 2.30 |
| 02:00 | 1447 | Toluca W vs Club Tijuana W | 2.58 | 3.75 | 2.25 |
| 02:00 | 3433 | Universidad Catolica vs Talleres | 2.56 | 3.29 | 2.47 |
| 02:05 | 1347 | Leon W vs Necaxa W | 1.67 | 3.80 | 4.18 |
| 06:10 | 3057 | CF Pachuca vs Puebla FC | 1.60 | 3.99 | 4.98 |
| 14:30 | 5964 | Perth Glory vs Brisbane Roar | 2.79 | 3.29 | 2.42 |
| 15:30 | 2773 | Thailand vs Malaysia | 1.43 | 3.99 | 6.62 |
| 16:15 | 3007 | United Arab Emirates vs Kuwait | 1.81 | 2.97 | 4.76 |
| 19:15 | 3674 | Qatar vs Bahrain | 2.81 | 2.76 | 2.62 |
| 20:30 | 2324 | Al Raed Club vs Al Hilal Riyadh | 5.99 | 4.60 | 1.46 |
| 20:30 | 4861 | Mamelodi Sundowns vs Chippa Utd | 1.35 | 4.35 | 9.30 |
| 20:45 | 3891 | Twente vs Telstar | 1.25 | 5.45 | 8.37 |
| 21:45 | 5933 | Leixoes vs Famalicao | 3.02 | 3.21 | 2.19 |
| 22:00 | 1985 | NAC Breda vs FC Eindhoven | 2.17 | 3.37 | 2.93 |
| 22:00 | 3878 | Lincoln vs Accrington | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 22:30 | 1755 | Wrexham vs Bromley | 1.30 | 5.12 | 8.28 |
| 23:00 | 4943 | Manchester Utd vs Charlton | 1.16 | 7.25 | 13.82 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# AZAM YASAJILI KIPA MGHANA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imetangaza kumsajili kipa Abdulai Iddrisu kutoka nchini Ghana kwa mkataba wa miaka miwili.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana mchana imeeleza kuwa imesajili kipa huyo akitokea Klabu ya Bechem United ya nchini humo.

"Tunayofuraha kuwataarifu kuwa tumefanikiwa kumsajili kipa mahiri kutoka Ghana, Abdulai Iddrisu, kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Bechem United ya kwao Ghana," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Azam FC imemsajili kipa baada tetesi kuwa inasaka kipa, siku moja tu ilipomalizika mechi yao dhidi ya Yanga Desemba 25, mwaka jana na kuchapwa mabao 3-2, huku mashabiki wengi wa soka wakimlaumu kipa raia wa Comoro, Ali Ahmada, kuwa alifungwa baadhi ya mabao kizembe.

Mashabiki, wadau wa soka na wachambuzi wakaenda mbali zaidi kuwa si mechi hiyo tu, bali mara kwa mara amekuwa akifungwa baadhi ya mabao ambayo hayakupaswa kutinga nyavuni kwa sifa ya kipa mkubwa kama yeye.

Kabla ya mechi hiyo, Azam ilikuwa inahusishwa kumchukua kipa Beno Kakolanya kutoka Simba, lakini ni kama vile dili hilo limeyeyuka.

Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, juzi alibainisha kuwa klabu yao itasajili wachezaji wanne kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo, watatu wa Kitanzania na mmoja wa kigeni.

"Kuna watu kama vile wanatukatia tamaa, lakini tarehe zenyewe za maumivu ni zile za mwisho za usajili, kuanzia terehe 13, 14 na 15 na ndani ya siku hizi mbili tatu, tutatangaza mchezaji wa kwanza tuliyemsajili kwenye dirisha dogo na hiki chuma kitatoka nje ya nchi.

"Tutasajili wachezaji wanne, mmoja kutoka nje ya nchi na watatu wa hapa nchini, nadhani mashabiki wa Azam FC wajiandae kupokea usajili huu ambao utakuwa ni pigo kwa upande mwingine, lakini kwa upande wetu ni furaha tu, mashabiki wanataka kuona timu ikifanya vema kwenye Ligi Kuu," alisema Ibwe siku moja kabla ya kumtangaza mchezaji huyo.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kushoto), akimtambulisha kipa mpya wa timu hiyo, Abdulai Iddrisu kutoka Ghana. **MPIGAPICHA WETU**

# ROBERTINHO AANZA KAZI, SIMBA SC WATULIZWA USAJILI

INATOKA UK. 24

kwenda Dubai na kudai fedha za safari hii tungezipeleka kwenye usajili, watu wasiwe na hofu kwani fedha za usajili ni zingine tofauti na safari ya Dubai, zoezi la usajili linaendelea chini ya Mwenyekiti, Salim Abdallah 'Try Again'.

"Wanasimba endeleeni kuwa watulivu hatuwezi kukubali kuingia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa bila ya kufanya usajili kwenye mapungufu tuliyokuwa nayo katika kikosi chetu," alisema Ahmed.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema wanajipanga vizuri kwa ajili ya kufanya vizuri katika raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema wanahitaji kufanya maandalizi mazuri hasa kuelekea katika michuano ya kimataifa kuhakikisha wanavuka katika hatua ya makundi na kusonga mbele.

"Tunaenda kwenye maandalizi tukiwa na malengo ya kuhakikisha kikosi kinarudi kikiwa na ubora mkubwa zaidi kwa ajili ya mashindano yaliyo mbele yetu," alisema Mgunda.

Alisema tayari wameanza majukumu chini ya Robertinho kuhakikisha wanafikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimba katika ligi ya ndani na michuano ya kimataifa.

Michezo
Jumatatu Januari 9, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Zidane akataa kuwa kocha wa Marekani

# ROBERTINHO AANZA KAZI, SIMBA SC WATULIZWA USAJILI

## ●●●Ni wakati akiendelea kuwajaza mbinu nyota wake huko Dubai, huku...

**Na Saada Akida, Zanzibar**

WAKATI Kocha Mkuu mpya wa Simba, Robertinho Oliveira, akianza kazi rasmi ya kukinoa kikosi hicho huko Dubai, Falme za Kiarabu jana, ikiwa ni baada ya wiki iliyopita kueleza kuvutiwa na wachezaji wanne waliocheza mechi mbili za Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar, uongozi wa klabu hiyo umesema "tulieni vyuma zaidi vinakuja".

Katika mechi mbili Simba ilizocheza kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi Robertinho akiishuhudia jukwaani, ilichezesha wachezaji ambao wamekuwa hawapati nafasi kikosi cha kwanza na kati ya hao, kocha huyo raia wa Brazil, aliwataja Denis Kibu, Jonas Mkude, Kennedy Juma na kinda Michael Joseph, kuwa waliomvutia zaidi akiamini wanahitaji kuongezewa vitu vichache kabla ya kutisha.

Robertinho ambaye anasaidiwa na Juma Mgunda pamoja na Selemani Matola, jana alianza rasmi kukinoa kikosi hicho huko Dubai kilipoweka kambi ya wiki moja kujiandaa na mechi za Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, wakati akiendelea kuwasoma nyota wake na kuwajaza mbinu zaidi, dirisha dogo la usajili bado lipo wazi na uongozi wa Simba umesema upo katika mchakato wa kukamilisha mazungumzo ya mwisho na baadhi ya wachezaji ili kuboresha kikosi chao hususan safu ya ushambuliaji.


Hadi sasa katika usajili wa dirisha dogo, Simba imemtambulisha, Saido Ntibazonkiza pekee ambaye amesajiliwa akitokea Geita Gold na katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu Bara akiwa na jezi ya Simba dhidi ya Tanzania Prisons, alihusika katika mabao manne, akifunga matatu 'hat-trick' na kutoa asisti moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kupitia dirisha la usajili wamejipanga vizuri na kuwashusha presha mashabiki wa Simba kuwa viongozi wako makini.

Alisema tayari benchi la ufundi limesheheni wataalamu baada ya ujio wa Robertinho na mchakato wa usajili unaendelea vizuri na kwamba watafanya usajili mkubwa sana katika nafasi zilizozipendekeza na benchi la ufundi.

"Kupitia dirisha hili la usajili, niwatoe hofu mashabiki wa Simba kuwa uongozi wetu upo makini, kuna baadhi ya watu wanasononeka sisi

INAENDELEA UK. 23



Robertinho Oliveira

## Nyota bora wanaoweza kusaini mikataba Januari



**LONDON, England**

DIRISHA la usajili la Januari 2023 lipo wazi na klabu zitatafuta kusajili mchezaji mmoja au wawili ili kuimarisha kikosi chao katikati ya msimu huu.

Hata hivyo, pia kuna baadhi ya wachezaji ambao wamebakiza miezi sita pekee katika mikataba yao ya sasa na wanaweza kusainiwa kwa makubaliano ya awali ya mkataba Januari.

UK. 14

## Mawinga 5-bora wa kushoto 2022



**LONDON, England**

SIKU zimepita wakati mawinga wa kushoto walikuwa mashine za kuvuka bila kuchoka. Mawinga wa kushoto wa zama za kisasa ni hodari zaidi, wenye uwezo wa kufanya mengi zaidi.

Wengi wa mawinga wa sasa wa kushoto wanaocheza kwa kasi kubwa, ni wazuri sana wakiwa na mpira miguuni mwao.

UK. 12

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >